


Awamu ya kwanza ya kusafisha ikiendelea ili kuanza ujenzi wa upanuzi wa barabara ya Morogoro kutoka Kimara Mwisho mpaka Ubungo, jijini Dar as Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Zitto kujitosa urais uchaguzi mkuu 2025

**Na Jenifer Gilla**

MWENYEKITI mstaafu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema yupo tayari kupeperusha bendera ya chama hicho katika nafasi ya urais wakati wa Uchaguzi Mkuu mwakani, endapo wanachama watampa ridhaa hiyo.

Alitoa kauli hiyo jana wakati wa sherehe za kutimiza miaka 10 ya chama hicho zilizofanyika mkoani Kigoma na kuhudhuriwa na wanachama, viongozi mbalimbali wa chama hicho kutoka Bara na Visiwani.

Zitto amekuwa akisikika akitangaza nia ya kuwania ubunge katika Jimbo la Kigoma Mjini alilowahi kuliongoza mwaka 2015 hadi 2020, lakini jana ilikuwa tofauti akisikika kutangaza kuwania urais.

Alisema licha ya kustaafu kwake kwenye uongozi hatosita kufanya jambo lolote litakalokuwa na maslahi ya chama na nchi endapo viongozi wataona anafaa kutumika katika jambo hilo.

"Nimejiandaa kisaikolojia, kiakili na kimaarifa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wowote viongozi wangu mkinihitaji nipo tayari kuwahudumia," alisema Zitto.

Kuhusu uamuzi wake wa kuingia katika kinyang'anyiro hicho, Zitto alisema utatokana na matakwa ya wananchi na kutimiza malengo ambayo chama hicho kimejiwekea kwa miaka 10 ijayo ikiwamo kushika dola na kuiletea nchi maendeleo.

Alisema wakati chama hicho kinaanzishwa watu walikiita ni chama cha wana Kigoma, lakini sasa kimekuwa na viongozi na wawakilishi nchi nzima, akisema ni jambo la kujivunia.

"Kiongozi wa chama ni mtu kutoka Kilimanjaro, Mwenyekiti ni mtu kutoka Pemba, Makamu Mwenyekiti Bara ni mtu kutoka Lindi, Makamu Zanzibar ni mtu kutoka Unguja, Katibu Mkuu katoka Tunduru. Wanachama mjivunie mbegu mliyoipanda kwa miaka 10 iliyopita kwa sasa imeenea Tanzania nzima mnapaswa kutembea kifua mbele," alisema Zitto.

Naye Mwenyekiti wa chama hicho, ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Massoud Othman, alisema msimamo wa chama hicho ni kuhakikisha kuwa kunapatikana Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi ili Watanzania wanakuwa na uhuru wa kumchagua rais wamtakaye.

Alisema ili hilo liwezekane chama hicho kinapaswa kuwa madarakani katika uchaguzi ujao na kuwasihi wanachama wa chama hicho kuhakikisha wanachagua viongozi wa chama hicho kwa kishindo katika uchaguzi ujao.

"Mungu akipenda mwaka 2025 tunataka tushindane na Kigoma, mkikabidhiwa serikali kule (Zanzibar) huku Kigoma pia (Bara) mtukabidhi kwa sababu ng'ombe hachinjwi mkiani," alisema.

**JUSSA AAHIDI USHINDI**

Makamu Mwenyekiti wa ACT Zanzibar, Ismail Jussa, alisema kwa upande wa Zanzibar wamejipanga kuhakikisha kuwa katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba mwakani chama hicho kitachukua madaraka chini ya Mwenyekiti wao, Othman Masoud Othman ili kuwaletea wananchi maisha wanayostahili.

Aidha, aliwataka wananchi wa Kigoma kuhakikisha kuwa wanampitisha Mwenyekiti mstaafu, Zitto Kabwe kuwa mbunge wa jimbo hilo pamoja na kumpitisha kwa kishindo katika nafasi ya urais katika Uchaguzi Mkuu mwakani.

# Kimbunga Hidaya kilivyoathiri watahiniwa kidato cha sita

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Taifa la Mitihani (NECTA) limetangaza kuanza kwa mitihani ya kidato cha sita na ualimu ngazi ya astashahada na stashahada, huku kimbunga Hidaya kikiathiri moja ya shule mkoani Lindi na watahiniwa kulazimika kutofanya mtihani huo kupitia kituo.

Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Dk. Said Mohamed, alitoa taarifa hiyo jana mkoani Dar es Salaam akisema mitihani hiyo itaanza leo hadi Mei 24 kwa kidato cha sita na ya ualimu itamalizika Mei 20, mwaka huu.

Dk. Mohamed aliitaja shule ambayo imeathiriwa na Kimbunga Hidaya kuwa ni Kilwa.

"Kutokana na Kimbunga (Hidaya) tumepokea taarifa ya athari kwa shule moja ya msingi ambayo hata hivyo, haihusiani na athari ya kuanza kwa mitihani inayokwenda kuanza kesho (leo)," alisema.

Dk. Mohamed alisema mitihani ya kidato cha sita itafanyika katika shule za sekondari 931 na vituo vya watahiniwa wa kujitegemea 258 na wa ualimu katika vyuo vya ualimu 99.

"Watahiniwa 113,504 wamesajiliwa kufanya mitihani ya kidato cha sita mwaka 2024 ambapo kati yao, watahiniwa wa shule ni 104,449 na wa kujitegemea ni 9,055," alisema.

Alisema kati ya watahiniwa wa shule waliosajiliwa, wavulana ni 57,378 sawa na asilimia 54.9 na wasichana ni 47,071 sawa na asilimia 45.1.

Dk. Mohamed alisema watahiniwa wenye mahitaji maalum ni 232 na kati yao, 201 ni wenye uoni hafifu, 16 ni wasioona na 15 ni wenye ulemavu wa viungo vya mwili.

Alisema kati ya watahiniwa wa kujitegemea 9,055 waliosajiliwa, wavulana ni 5,515 sawa na asilimia 60.91 na wasichana ni 3,540 sawa na asilimia 39.09.

Alisema watahiniwa wa kujitegemea wenye mahitaji maalum wako watatu ambao wote ni wenye uoni hafifu.

"Mwaka 2023 idadi ya watahiniwa wa shule na wa kujitegemea waliosajiliwa walikuwa 106,883, hivyo kuna ongezeko la watahiniwa 6,621, sawa na asilimia 6.19 kwa mwaka 2024 ukilinganisha na mwaka 2023," alisema Dk. Mohamed.

Kuhusu mitihani ya walimu, Dk. Mohamed alisema watahiniwa 11,552 wamesajiliwa kati yao 2,766 ni wa ngazi ya stashahada na 8,786 ni wa ngazi ya cheti.

Alisema ngazi ya stashahada, wanaume ni 1,634 sawa na asilimia 59.07 na wanawake ni 1,132 sawa na asilimia 40.93. Aidha, ngazi ya cheti watahiniwa 3,969 sawa na asilimia 45.17 ni wanaume na 4,817 sawa na asilimia 54.83 ni wanawake.

Watahiniwa wenye mahitaji maalumu waliosajiliwa ni 12 wenye uoni hafifu ni wawili kwa ngazi ya stashahada na wanane kwa ngazi ya cheti. Watahiniwa wasioona kwa ngazi ya cheti ni wawili.

Kwa mujibu wa Dk. Mohamed, mwaka jana idadi ya watahiniwa wa ualimu waliosajiliwa walikuwa 8,479, na kuna ongezeko la watahiniwa 3,073 sawa na asilimia 36.24 kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na mwaka 2023.

Alisema pamoja na maandalizi yote muhimu yaliyofanyika kamati za mitihani za mikoa na halmashauri zinapaswa kuhakikisha usalama wa vituo unaimarishwa.

"Baraza linatoa wito kwa wasimamizi wote walioteuliwa kusimamia mitihani kufanya kazi yao kwa weledi na uadilifu wa hali ya juu. Wazingatie kanuni za mitihani na taratibu, miongozo ya baraza waliyopewa ili kila mtahiniwa apate haki yake," alisema.

Aidha, Dk. Mohamed alitoa wito kwa wakuu wa shule kutekeleza majukumu yao ya usimamizi kwa kuzingatia mwongozo wa usimamizi uliotolewa na NECTA na kuepuka kuingilia usimamizi wa watahiniwa ndani ya vyumba.

Kadhalika, alisema NECTA linawaasa wamiliki wa shule kutambua kuwa shule zao ni vituo maalum vya mitihani na hivyo hawatakiwi kuingilia majukumu ya wasimamizi wa mitihani katika kipindi chote cha ufanyaji wa mitihani hiyo.

Alisema baraza litachukulia hatua mtu yeyote atakayebainika kujihusisha na kusababisha udanganyifu kwa mujibu wa sheria.

TANGAZO


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422



Meneja Uhusiano wa Taasisi za Serikali wa Benki ya Azania, Halima Semhunge, akitoa maelezo kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Prof. Kitila Mkumbo (katikati) akiwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Tausi Kida, wakati wa uzinduzi wa kituo cha kisasa cha kutolea huduma kilichoko ndani ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwenye hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Gilead Teri. **PICHA: MWANDISHI WETU**

# 6 mbaroni tuhuma kujihusisha na mikopo ya kausha damu

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi mkoani Songwe kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), limewakamata watuhumiwa sita wanaojihusisha na utoaji wa mikopo ya kausha damu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Songwe, Augustino Senga, alisema watu hao wamekamatwa wakifanya biashara ya kutoa mikopo bila ya kuwa na leseni kinyume cha Sheria ya Mikopo Midogo Namba 10 ya Mwaka 2018, Kifungu cha 16.

Senga alisema watuhumiwa hao wamekamatwa baada ya Jeshi la Polisi kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu huduma za mikopo midogo maarufu kama kausha damu wanayoifanya.

Alisema baada ya kupokea malalamiko hayo waliendesha operesheni ya kukusanya ushahidi na kuwakamata wamiliki wa kampuni na watu binafsi wanaotoa huduma za kifedha pasipo kuwa na leseni.

Kamanda Senga alisema watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria na atakayepatikana na hatia atalipa faini isiyopungua Sh. milioni 20, lakini isiyozidi Sh. milioni 100 au kifungo kisichopungua miaka mitano jela.

Kadhalika, aliwakumbusha watoa huduma wa mikopo midogo kufuata taratibu za usajili na miongozo iliyowekwa na BoT ili kuepuka usumbufu unaotokana na kutotii sheria.

Vilevile, alitoa wito kwa wananchi wa mkoa huo kuwabaini na kuwakamata wafanyabiashara ambao wanaochukua kadi za benki kama dhamana ya mikopo hiyo kinyume cha sheria.

Katika tukio lingine, Kamanda Senga alisema Jeshi la Polisi liliwakamata watuhumiwa sita kwa tuhuma za kughushi barua ya kusitishiwa mikataba ya kazi ikiwa na mihuri ya taasisi binafsi na za serikali pamoja na fomu za kuchukulia mafao ili waweze kujipatia pesa kwa njia ya udanganyifu.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa Februari 22, mwaka huu na upelelezi wa mashauri haya bado unaendelea na utakapokamilika watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi.

### SERIKALI YAHADHARISHA

Hivi karibuni serikali kupitia Ofisa Mkuu Mwandamizi Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Salim Kimaro, ilitoa wito kwa watoa huduma za kifedha nchini kufuata sheria na taratibu za huduma za fedha ikiwamo kupata leseni ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ili kuhakikisha huduma hizo zinatolewa kwa ufanisi bila kuwaumiza na kuwadhalilisha wanufaika na hatimaye kukuza uchumi wa nchi.

Benki hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha imeona umuhimu wa kutoa elimu ya fedha nchi nzima ili kuwapa uelewa wananchi kuhusu namna bora ya kukopa fedha na kurejesha mkopo bila kudhalilishwa.

Serikali imebaini kuwa mikopo inayotolewa kwa njia ya mitandao ya simu ni changamoto kubwa hasa katika ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wakopaji jambo linalosababisha watoa huduma hao kuvunja sheria ya usiri inayotakiwa katika kupata huduma ya fedha kwa kuwadhalilisha wakopaji hao kwa kutuma ujumbe mfupi kwa ndugu na jamaa waliochukua mikopo hiyo.

"Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania tunahitaji kushirikisha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, kampuni za simu na Polisi ili kuona namna ambayo tunaweza kulitatua suala hili la udhalilishaji linalofanywa na watoa huduma za fedha kupitia mitandao ya simu," ilisema serikali kupitia ofisa huyo.

Aidha, Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania hivi karibuni itaendesha kampeni kupitia vyombo vya habari na njia mbalimbali za kutoa elimu kwa umma ili kujenga uelewa kwa wananchi na watoa huduma ndogo za fedha kuhusu masuala muhimu ya kuzingatia katika utoaji na upatikanaji wa huduma ndogo za fedha nchini.

### WAATHIRIKA MIKOPO UMIZA

Waathirika wa mikopo hiyo watajwa kuwa ni wastaafu na walimu kutokana na madai ya kipato wanachopata kutoridhisha na hivyo kujiingiza kwenye mikopo hiyo na mwishoe kuishia udhalilishaji.

Hivi karibuni mjadala uliibuka bungeni kutoka kwa wabunge wakilaani mikopo hiyo na kuta serikali ichukue hatua za haraka.

Kadhalika, alisema Jeshi la Polisi linawashikilia watuhumiwa 11 kwa makosa ya wizi wa pikipiki nne, pamoja na kuwakamata watuhumiwa wengine 14 kwa makosa ya uvunjaji.

Pia, alisema Jeshi la Polisi linawashikilia watuhumiwa 424 kwa kujihusisha na matukio ya ukatili wa kijinsia, uvunjaji, wizi, mauaji, utapeli kwa njia ya mtandao, kujifanya mtumishi wa serikali, kughushi nyaraka, dawa za kulevya, ukiukwaji

# Kinana ataja siri 4 ushindi uchaguzi mkuu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana ametaja siri nne za ushindi kwenye uchaguzi; mojawapo ni sera nzuri za chama, huku akisema madai ya Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi sio kigezo pekee cha kushinda.

Aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akizungumza na wananchi, akizitaja siri hizo ni sera nzuri za chama, kukubalika kwa chama, wagombea wazuri na kujipanga kwenye uchaguzi.

"CCM hatukatai na Watanzania wanaitaka Katiba. Kimsingi Katiba mpya hatuikatai lakini wenzetu (CHADEMA) wanataka Katiba leo," alisema Kinana.

"Hatukatai kukosolewa (CCM), kusahihishwa, lakini hatukubali kushtumiwa kwa mambo ambayo hayapo, kubwa walilofanya kwenye mizunguko yao (CHADEMA) ambalo walidhani ni kubwa ni kujenga chuki, mfarakano miongoni mwa Watanzania, hiyo ndio ilikuwa ajenda yao kubwa."

Aidha, alisema moja ya hoja zilizopelekwa na baadhi ya vyama vya upinzani ni Rais asiwe na mamlaka ya kuteua tume, jambo ambalo hata CCM iliunga mkono.

"Hakuna lililopendekezwa la msingi ambalo tumelikataa, bado CHADEMA wanasema Rais asihusishwe kwenye kuteua Mwenyekiti, sijaona nchi ambayo Rais hahusishwi kwenye uteuzi wa tume, hawa wanataka kumuweka kando Rais," alisema Kinana.

Aidha, alisema walipokuwa wanazungumza suala la Katiba mpya (CHADEMA) walikuja na hoja kwamba liwe suala la CCM na CHADEMA kitu ambacho kilisababisha wasikubaliane.

Alisema hoja ya chama hicho ni kwamba wao ni chama kikuu cha upinzani na vyama vingine viwekwe kando jambo ambalo sio sawa.

Kuhusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Kinana alisema ni wa mfano na hakuna kama huo duniani licha ya kupitia majaribio, kashkashi nyingi, lakini umedumu kutokana na waasisi kujenga misingi bora.

"Tusikubali Watanzania kugawanywa kwa maeneo, baadaye tutagawanywa kwa dini, mambo yanaanza polepole ya kugawanya watu, Watanzania tuendelee kuikataa hoja hii, nchi nyingi duniani hazina mfumo wa majimbo zina mfumo wa umoja."

Alisema CCM itazingatia sheria, kanuni na matarajio ya Watanzania katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka huu na ule mkuu wa mwakani.

HABARI KITAIFA

# Marubani ATCL wakodiwa kufundisha Nigeria



Marubani waandamizi wa Kampuni ya Ndege Tanzania, Kapteni Sajjad Moloo (kulia) na Kapteni Arif Jinnah (kushoto), wakiwa ndani ya ndege kwa ajili ya mafunzo kwa walimu na marubani wa ndege ya Ibom, nchini Nigeria. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya Ndege Tanzania (ATCL) imeingia makubaliano ya kupeleka marubani wake kufundisha na kusimamia ndege mpya za Airbus A220 za Kampuni ya Ndege ya Ibom iliyopo nchini Nigeria.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Ladislaus Matindi jana alisema kuwa kampuni yake imetoa marubani wake waandamizi wawili.

Matindi, alisema marubani hao watakuwa na jukumu la kuwafundisha kwa vitendo marubani na walimu wa marubani wa Ibom Air kwa muda wa miezi sita.

"Marubani wa ATCL watakuwa na jukumu la kufundisha na kusimamia mafunzo kwa vitendo hadi watakapojiridhisha kuwa marubani wanafunzi na walimu wao wamefikia viwango vinavyotakiwa kurusha ndege hizo," alisema.

Aidha, alisema Ibom Air itailipa ATCL gharama za mafunzo hayo kwa mujibu wa mkataba kwa kipindi chote cha makubaliano.

Alisema makubaliano hayo yamefikiwa baada ya ATCL kuonesha uzoefu wa muda mrefu wa kumiliki ndege za Airbus A220-300 na pia kuridhishwa na kiwango cha umahiri wa marubani wa Air Tanzania.

Mafunzo hayo yanalenga kujenga uwezo kwa marubani wa Ibom Air watakaorusha ndege za Airbus A220, ambazo ATCL ina uzoefu wa miaka mingi wa kumiliki ikilinganishwa na Ibom Air ambao ndio wanaanza kutumia ndege za aina hiyo.

Miongoni mwa mafanikio makubwa ya ATCL, ni kuwa na ndege ya mizigo ya Boeing 767-300F ambayo imeanza safari za kwenda nchi mbalimbali ikiwamo Guangzhou China.

Hivi karibuni Matindi alisema kuwa wako kwenye maandalizi ya kuanza safari za kuelekea moja kwa moja London, Uingereza kwa kutumia ndege yake ya Boeing 787-8 Dreamliner.

Pia, alisema wanatarajia kuendelea kuongeza miruko ya kwenda Mumbai, India na Guangzhou, China na kuanzisha safari mpya za Dubai, Muscat, Lagos Nigeria, Kinshasa na Goma Congo DRC.

Akizungumzia huduma mpya ya Air Tanzania App, Matindi, alisema ni huduma inayopatikana kwenye simu za aina zote zinazotumia mifumo ya "android" na zile za "ios". Alisema Air Tanzania App inamleta msafiri kwenye ulimwengu halisi wa wasafiri wa anga na kumpa uzoefu wa pekee wa faragha na uhuru wa kuchagua.

"Air Tanzania App sio tu kwa ajili ya kuwezesha safari bali inamwezesha mteja wa Air Tanzania kunufaika na ofa za bidhaa mbalimbali pamoja na kupata huduma za nyongeza," alisema.

"Kupitia Air Tanzania App, mteja ataweza kuchagua muda wa safari, daraja la safari, kiti, kununua begi la ziada mahali popote alipo, muda wowote anapohitaji kusafiri kwenda sehemu yoyote ndani na nje ya nchi ambapo Air Tanzania inafanya safari zake," alisema.

Alisema mteja anayetumia Air Tanzania App ataweza kulipia na kupata tiketi yake ya safari papohapo ambapo kwa sasa wateja watapatiwa huduma kwenye vituo 15 vya ndani ya nchi na 11 nje ya nchi.

"Tunakusudia kuongeza vituo vya Pemba, Tanga, Mafia, Nachingwea na Musoma na kurudisha safari za Iringa na Mtwara kwa mtandao wa safari za ndani ya nchi ili kuwawezesha wadau wengi kunufuaika na Air Tanzania," alisema.

BANK OF AFRICA
BMCE GROUP

TAARIFA KWA UMMA

**Bi. Esther Cecil Maruma -Mkurugenzi Mkuu
Bank of Africa Tanzania Limited**



Kwa furaha napenda kuutangazia umma kuteuliwa kwa Bi. Esther Cecil Maruma kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Bank of Africa Tanzania Limited, kuanzia tarehe 6 Mei, 2024. Bi. Maruma, ana uzoefu na utaalamu mkubwa alioupata kutokana na kuwa na taaluma na uzoefu wa muda mrefu katika sekta ya kibenki,moja ya nafasi kubwa aliyokuwa anashikilia hivi karibuni alikuwa ni Mkurugenzi wa Masoko ya kifedha ya kimataifa akiwa Absa Bank (T) Limited.

Kwa zaidi ya miaka 15 ya uongozi madhubuti na wa kuigwa, Bi. Maruma, anaendelea kuweka alama katika sekta ya huduma za kifedha. Uongozi wake wenye maono amefanikisha kukuza masuala ya hazina, masoko ya kifedha, biashara na uwekezaji wa kibenki kwa kiwango cha juu. Mafanikio yake makubwa ni pamoja ni kuwa kinara katika mikakati ya kibunifu ya kuongeza mauzo na masoko katika kuchochea kuongezeka kwa wateja, uboreshaji wa utoaji wa bidhaa na huduma, na kuweka mazingira ya kudhibiti hasara ambao umeleta ufanisi mkubwa katika ongezeko la mtaji na kukuza mizania.

Dhamira ya kujitoa ya Bi. Maruma katika kufanikisha ukuaji endelevu, kukuza na kuendeleza rasilimiali watu, mawazo na dhamira yake katika sekta kunadhamiria kuleta mabadiliko chanya ya kibiashara. Kutokana na dhamira na uzoefu wake wa kazi ambao utachochea ukuaji na ubunifu kwa Bank of Africa Tanzania Limited.

Bodi ina mani kubwa kutokana na ufahamu na uzoefu wa Bi. Maruma wa kuiongoza Benki katika kufikia malengo muhimu ya kimkakati. Tunaamini uongozi wake utachochea kasi ya masuala ya ujumuishaji katika sekta ya fedha, kukua kwa wafanyabiashara wa kati na wadogo (SME) nakuendeleza juhudi za kuleta mabadiliko ya kidijitali.

Bi. Maruma ana elimu ya Shahada ya Kwanza ya Sayansi katika Sayansi ya Mazingira na Uongozi kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, ikiongezea katika uzoefu wake wa muda mrefu wa masuala ya uongozi na utendaji.

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, natoa pongezi za dhati kwa Bi. Maruma kwa kuteuliwa kwake. Tuna imani kwamba uongozi wake wenye maono utaleta mafanikio chanya katika sekta na pia wadau wetu wote.

**NEHEMIAH KYANDO MCHECHU
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi
Bank of Africa Tanzania Ltd**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi chezesheni kwa haki kuelekea kumaliza msimu wa ligi

**WAKATI** Ligi Kuu Bara ikiwa imebakisha raundi tano tu kutamatika, bado kuna uchezeshaji usioridhisha kwa baadhi ya waamuzi. Kwa bahati mbaya sana uchezeshaji huo unaangukia kwa timu zinazosaka ubingwa, huku zile zinazotafuta nafasi ya nne ili zicheze mechi za kimataifa mwakani, au zinazokimbia kushuka daraja, zikionekana kukandamizwa zaidi.

Kumekuwa na baadhi ya matukio yanaonekana kujirudia kwa waamuzi, wakizinufaisha timu zingine na kuziumiza zingine, ambapo baadaye mamlaka husika inakuja kugundua kuwa ni makosa.

Mfano, katika mechi ya Aprili 27, mwaka huu kati ya Yanga na Coastal Union, uliochezwa, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, mchezaji Lameck Lawi wa Coastal Union alionyeshwa kadi nyekundu kwa kile kilichoelezwa kumvuta jezi Stephane Aziz Ki.

Hata hivyo, Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), ilipokea taarifa za uchambuzi wa kitaalamu kutoka kwa wakufunzi wa waamuzi, ambazo zimeainisha kuwa mchezaji huyo hakustahili kuonywa kwa kadi nyekundu, badala yake ilipaswa aonyeshwe kadi ya njano kwa sababu wakati tukio linatokea kulikuwa na mlinzi mwingine wa Coastal Union mbele yake ambaye angeweza kuufikia mpira.

Mwamuzi Rafael Ikambi aliyemwonyesha mchezaji huyo kadi nyekundu na msaidizi wake namba mbili, wakapewa onyo kali. Wakati akionyeshwa kadi timu hizo zilikuwa suluhu, lakini baada ya hapo Yanga ilipata bao 1-0.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza kati ya timu hizo mbili, iliyochezwa Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, mwamuzi Emmanuel Mwandimbwa, pia alimtoa nje kwa kadi nyekundu mchezaji Semfuko Charles, Yanga ikishinda bao 1-0, lakini Kamati pia iliifuta kadi hiyo baada ya kujiridhihirisha kuwa haikustahili. Mwamuzi huyo alifungiwa miezi sita.

Februari mwaka huu, Bodi ya Ligi ilimfutia adhabu mchezaji wa Prisons, Zabona Mayombya, alipoonyeshwa kadi nyekundu na mwamuzi Ahmed Arajiga katika mechi ambayo timu hiyo ilicheza na Yanga, Februari 11.

Hatutaki kusema kwa nini mechi zote ambazo wachezaji wanaoonyesha kadi nyekundu na waamuzi na baadaye zinafutwa ni za Yanga, kwa sababu mchezaji anapofanya madhambi ni lazima aadhibiwe, lakini tunajiuliza kwa nini huwa zinafutwa baadaye? Ina maana waamuzi wanatoa kadi kwa mihemko. Kwa nini huwa hawajiridhishi kwanza? Kwa nini mara nyingi zinazoumizwa ni timu ndogo? Kwa nini waamuzi huwa hawakosei kuwatoa kwa kadi nyekundu wachezaji wa timu kubwa halafu baadaye zikafutwa?

Hii inaonyesha kabisa hizi timu kubwa pamoja na kuwa na wachezaji bora, wenye uwezo mkubwa, wanalipwa mamilioni ya pesa, lakini wakati mwingine timu zao zinashinda kwa msaada wa waamuzi, huku timu zinazoitwa au kujiita ndogo zikizidi kuonewa.

Hata wakiadhibiwa waamuzi kwa makosa, lakini timu hizo zinakuwa zimeshaathirika kwa kupoteza pointi ambazo wakati mwingine zitakuja kuwahukumu mwishoni mwa ligi.


Hivyo, rai yetu ni kuelekea msimu ujao, Bodi ya Ligi itunge kanuni ya kutoa adhabu kali zaidi kwa waamuzi hususan kuwasimamisha kwa msimu mzima wanaotoa adhabu kama hizo bila kujidhihirisha pasipo shaka.

Mara nyingi, watoa haki, mahakimu, au waamuzi wanaambiwa wanapotoa adhabu, hasa zile zinazokuwa na athari za moja kwa moja, wanatakiwa wajidhihirishe pasipo shaka, na iwapo kuna shaka, basi wasifanye hivyo. Ni bora kumuachia mtuhumiwa huru, kuliko kumfunga mtu asiye na hatia.

Waamuzi nao wanatakiwa kuzingatia kuwa ni bora kutotoa kadi nyekundu kama hana uhakika, kuliko kumtoa mchezaji nje wakati hastahili. Huu ni uonevu mkubwa na haupaswi kufumbiwa macho.

Tunapoelekea mwishoni kumalizia mechi za ligi, tunatamani kuona waamuzi wakiongeza umakini zaidi, ili kutompa mtu ubingwa usiostahili, au kuishusha timu daraja ambayo haikutakiwa kwenda Ligi ya Championship, ila kwa sababu ya uamuzi wao tu wa mihemko.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# TFF, Bodi itolee ufafanuzi tuhuma timu kupuliziana dawa vyumbani

Na Adam Fungamwango

**KWA** muda mrefu sasa kumekuwa na tuhuma za timu za Ligi Kuu kuwekeana kile kinachodaiwa kuwa ni dawa za kunyong'onyesha nguvu za wachezaji katika vyumba vya kuvalia.

Awali, ilionekana kama ni jambo tu la kupita, lakini kwa sasa limeanza kuwa gumzo, na kuonekana kama ni jambo au habari za kawaida tu kwenye soka letu ambalo linapiga hatua kila kukicha.

Hata hivyo, wakati soka la Tanzania linapiga hatua, lakini kuna vitu ambavyo vinaonekana kulichafua soka letu.

Kwanza kabisa ni imani za kishirikina ambapo hivi karibuni, Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara imezipiga faini Klabu za Simba, Yanga, Mashujaa FC na Prisons kwa vitendo vinavyoashiria kuwa ni ushirikina.

Inashangaza kuona katika karne hii ya 21, bado klabu haziamini kuwa na wachezaji bora, benchi la ufundi zuri na uongozi bora ili kupata matokeo.

Bado hadi leo klabu kubwa kama Simba na Yanga zinakacha kupita mlango rasmi, na kupenya katika milango mingine ili kukwepa kile wanachokiita uchawi.

Inashangaza kuona eti TFF ikilalamika kuwa Yanga imekuwa ikifanya hivyo ikicheza mechi dhidi ya Simba tangu msimu wa 2021/22, 2022/23 na msimu huu. Walichofanya wakaiongezea faini tu kutoka Sh. milioni moja hadi tano.

Hata wachezaji nao wamekuwa na akili hiyo hiyo kama ya viongozi wao.

Bakari Selemani na Abdallah Denis wa Coastal Union, pamoja na wa Namungo, James Mwashinga, hawakuingia kwenye vyumba vya kuvalia wakati wa mapumziko, timu zao zilipokutana Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, Aprili 17, Namungo ikishinda bao 1-0, jambo ambalo limehusishwa na imani za kishirikina.

Imefika wakati sasa, Shirikisho la Soka nchini (TFF), pamoja na kutoa adhabu ya faini ambazo nadhani zinainufaisha, lakini pia izikate timu pointi walau moja kwa kila kitendo kwa ajili ya kupunguza imani hizi, vinginevyo kuna msemo wa kiswahili unaosema usipoziba ufa utajenga ukuta.

Nirudi kwenye pointi ya kupulizia dawa vyumbani, hivi sasa limekuwa likitamkwa waziwazi, na baadhi ya timu zikisusa kuingia vyumbani, badala yake kukaa nje.

Inadaiwa wachezaji wanapoingia vyumbani, wanapokwenda uwanjani wanakuwa kwenye wakati mgumu kwani wanaishiwa nguvu pamoja na pumzi, hivyo kutokuwa na uwezo wa kupambana kama wenzao, badala yake wanakuwa na uwezekano wa kupoteza mechi hiyo, hata kwa idadi kubwa ya mabao.

Kwa sasa hata timu zinazocheza Ligi ya Championship zinatuhumiana kuwekeana dawa vyumbani.

Hivi karibuni tumeona baadhi ya timu zinaingia kwenye vyumba vya kuvalia Uwanja wa Benjamin Mkapa wakiwa na feni za kawaida, wakiepuka kuwasha vipoza hewa kwa madai kama hayo. Cha kushangaza hadi leo TFF na Bodi ya Ligi wamekaa kimya, kana kwamba wamebariki uwapo wa jambo hilo, au tuhuma zake.

Kitendo cha hata vyumba vya Uwanja wa Benjamin Mkapa, kutuhumiwa na jambo hilo halileti picha nzuri.

Ni wajibu sasa wa TFF na Bodi ya Ligi kuibuka na kueleza ukweli juu ya jambo hili. Ni kweli lipo? Kama lipo wanachukua hatua gani kulikomesha? Kama hakuna kwa nini kumekuwa na tuhuma hizi kwa muda sasa?

Ifike wakati sasa TFF iwe na madaktari wao, au iagize kutoka kwenye hospitali za serikali au binafsi kwa gharama za klabu husika, kwa ajili ya kupima hewa kwenye vyumba vya kuvalia kabla ya mechi za ligi kwa kushirikiana na wale wa klabu husika ili kuondoa sitofahamu hii.

Vinginevyo Ligi ya Tanzania itakuwa na sifa mbaya kwenye mataifa mbalimbali kuwa timu zinashinda kwa sababu ya kupulizia dawa wenzao vyumbani na si soka la uwanjani.

HABARI KITAIFA

# Majaliwa aagiza wadau afya kuboresha afya ya mama

**Na Sabato Kasika**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza watumishi wa Wizara ya Afya, wadau wa afya na jamii kushirikiana kuboresha huduma ya afya ya mama nchini.

Majaliwa alitoa maagizo hayo katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wakunga Duniani jijini Dar Salaam jana.

Alisema ni muhimu watumishi hao washirikiana na vyama vya kitaaluma kama Chama cha Wakunga Tanzania (TAMA) kwa kuwa wadau muhimu katika afya nchini.

Alisema huduma za ukunga zinahitaji ushirikiano kati ya wadau hao na jamii kwa kuzingatia kuwa kila aliyezaliwa amepitia mkononi mwa wakunga.

"Hivyo ninaagiza kwamba shirikianeni ili kuboresha huduma ya afya kwa ajili ya kupunguza idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi," alisema Majaliwa.

Alifafanua kuwa kutokana na huduma zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau, vifo wakati wa kujifungua, vimepungua kutoka 558 mwaka 2015/16 hadi kufikia 104 mwaka 2022.

"Hiyo yote imetokana na huduma nzuri ambazo zinaendelea kutolewa na serikali katika jamii, hivyo tuendelee kushirikiana," alisema Waziri Mkuu.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Rais wa TAMA, Beatrice Mwilike, aliiomba serikali kutengeneza mfumo wa kuwezesha wakunga kuhudumia wajawazito wakati wa kujifungua na watoto wachanga.

Alisema wakunga wanatakiwa kujengewa uelewa kuhusu mabadiliko ya tabianchi, athari zake kwenye afya ya uzazi, jinsi ya kuwahudumia waathirika na kuzuia matatizo yatokanayo na athari hizo.

"Tunaomba serikali kutambua taaluma ya ukunga katika utumishi wa umma kwani wahitimu bado wanaajiriwa kwa cheo cha Ofisa Muuguzi kitendo kinachopunguza morali wa kufanya kazi," alisema Beatrice.

Naibu Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), Tanzania, Melissa Barret, alisema shirika hilo limezindua mradi wa 'Thamini uzazi salama'. Kwa mujibu wa Melissa, mradi huo wa miaka saba utatekelezwa katika mikoa ya Dar es Salaam na Shinyanga.

"Mradi huu unalenga kuboresha na kuwezesha wakunga wataalamu Tanzania, ambao ni baina ya Serikali ya Tanzania Umoja wa Mataifa (UN)na Serikali ya Canada," alisema.

Alisema ni muhimu kuwa na wakunga wataalamu na ndio sababu wameamua kuendesha mradi huo na wanatarajia kuelimisha wakunga ili waweze kuboresha kazi zao na kuwa na uzazi salama zaidi.

"Ni ukweli usiopingika kuwa wakunga wataalamu ni watu wa muhimu katika afya ya mama na mtoto ili kupunguza vifo vya wajawazito na watoto," alisema.

Mwakilishi wa Balozi wa Canada nchini, Hellen Fytche, alisema nchi yake ina ushirikiano mzuri ya Serikali ya Tanzania na ni mdau mkubwa wa afya ya mama na mtoto na kwamba ndio sababu imetoka Dola bilioni 12 ili kufanikisha mradi huo.

"Mkunga mtaalamu ni nguzo ya afya ya mama na mtoto, hivyo ninaamini mradi huu utasaidia kuwaongezea ujuzi wakunga na kufanya kazi yao kwa weledi zaidi," alisema Fytche.



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, akiwasha bajaji kuzindua kampeni ya utunzaji wa mazingira chini ya Watu Credit Tanzania Ltd, kupitia ufadhili wa bajaji zinazotumia mfumo wa gesi asilia (CNG), jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mkurugenzi Mkazi wa Watu Credit Tanzania, Rumisho Shikonyi (nyuma) na (kushoto) ni Mkuu wa Biashara kutoka Kampuni ya TVS, Jonathan Masanja. **PICHA: JOHN BADI**

# Pacha wafariki dunia nyumba ikiteketea moto

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WATOTO wawili pacha, Bright na Brown George Banzi, wenye umri wa miaka mitano, wamefariki dunia na ndugu yao mwingine kujeruhiwa baada ya nyumba walimokuwa wamelala kuteketea kwa moto unaodaiwa kutokana na hitilafu ya umeme. Ofisa Habari Msaidizi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, Benjamin Bandula, amethibitisha watoto hao kufariki dunia na kumtaja aliyejeruhiwa kuwa ni Kulwa George Banzi, mwenye umri wa miaka tisa baada ya kujiokoa kwa kutoka nje ya nyumba hiyo.

Bandula, alisema tukio hilo lilitokea Jumamosi iliyopita majira ya saa mbili usiku Mtaa wa Kibao cha Shule Kata ya Kihonda, Manispaa ya Morogoro.

Alisema taarifa za tukio la nyumba hiyo kuungua, zililiripotiwa na Jeremia Majinja.

Alisema Majinga, aliliambia jeshi hilo kuwa nyumba hiyo yenye vyumba vinne inayomilikiwa na George Banzi, inateketea kwa moto na inadaiwa kuwa chanzo cha tukio hilo kwa mujibu wa mashuhuda inawezekana ni hitilafu ya umeme kwa kuwa ulikuwa unakatika na kurudi kila mara.

Alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo halisi cha tukio hilo na kuahidi kutoa taarifa baada ya kukamilika.

Vilevile Bandula, alisema wanaendelea kufanya uchunguzi ili kubaini madhara na thamani ya mali zilizotokea ikiwa ni pamoja na nyumba hiyo na samani za ndani baada ya kuteketea kwa moto.

Awali, alisema nyuma hiyo imeteketea kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza ikiwamo jeshi hilo kuchelewa kupata taarifa za tukio hilo na ubovu wa miundombinu ya barabara uliosababisha gari lao kuchelewa kufika kwa wakati.

"Ni kweli kioo cha mbele cha gari kimepasuliwa, mashuhuda waliougundua moto ukiwa umeshika sehemu kubwa ya nyumba, wananchi wakati wakijaribu kuuzima wenyewe baadaye wakatoa taarifa kwetu wakati moto ulikuwa umeshasambaa kwenye nyumba yote," alisema Bandula.

Wakazi wa eneo hilo walihamaki na kujaribu kushambulia gari la Zimamoto wakidai limechangia kuteketea kwa nyumba hiyo baada ya kuchelewa kufika katika eneo la tukio.

Tukio hilo lilidhibitiwa na askari wa Jeshi la Polisi na viongozi wa serikali ya mtaa huo waliokuwa eneo la tukio baada ya kuwatuliza wakazi hao.

# Serukamba ajivunia mafanikio ya kilimo Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Peter Serukamba, amewaasa viongozi mkoani hapa kuweka mkazo katika matumizi ya mbolea kwenye kilimo kwa kuwa ndio njia pekee ya kuwaondoa wananchi kwenye umaskini na kuongeza uzalishaji wa mazao.

Akizungumza katika hafla ya kumuaga iliyofanyika mjini Singida juzi mjini hapa, Serukamba, alisema mwaka 2022 Singida ilitumia tani 220 za mbolea na kiwango kikaongezeka na kufikia tani 6,400 mwaka jana jambo ambalo kama mkuu wa mkoa huo kwa vipindi hivyo aliona amefanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Alisema ameshangaa baada ya kuhamishiwa Iringa amekuta mwaka jana katika mkoa huo, walitumia tani 36,000 za mbolea kati ya lengo ka kutumia tani 42,000.

"Nikuombe dada yangu Halima (Halima Dendego) Mkuu wa Mkoa wa Singida hili la mbolea lipe fursa ndio 'game change' ya maendeleo ya watu wa Singida," alisema Serukamba.

Alisema bahati nzuri ni kwamba serikali imeweka fedha kwenye mbolea ili watu waweze kununua kwa bei ambayo ni nusu, hivyo hakuna sababu ya kutowafanya wakulima wasitumie mbolea kwenye kilimo.

Naye Dendego, alimshukru Serukamba kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kusimamia maendeleo wakati akiwa Singida kwani kila sehemu ameacha alama.

"Nimeshamaliza wilaya zote, nimepita halmashauri zote nimekuta alama yako kila ninapokanyaga, umefanya kazi kubwa sana, umesukuma sana miradi na mimi naungana na wanasingida pale pale ulipoachia kaka yangu ili tusonge mbele," alisema. "Yeye (Serukamba) ni baba mimi ni mama tunaweze tusifanane katika staili ya uongozi, lakini tutafanana katika malengo ya mafanikio, ukiona tunasukumana ndugu zangu ni katika kazi nje ya hapo ukitimiza wajibu wako mimi ni dada, mimi ni mama na mimi ni rafiki, sina historia ya kugombana na mtu," alisema.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Wanaohama Ngorongoro wakumbushwa kufuata utaratibu

Na Jenifer Gilla

WAKAZI wanaoishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro wametakiwa kufuata taratibu za serikali ili wapate stahiki zao zote kwa mujibu wa sheria na kufurahia maisha katika makazi yao mapya.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, Murtallah Mbillu, aliyasema hayo, mwishoni mwa wiki wakati akiaga kaya 105 zenye watu 564 na mifugo 1,540, kutoka katika hifadhi hiyo kuelekea Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, Wilaya ya Simanjiro (Manyara), Meatu (Shinyanga), Monduli (Arusha) na Morogoro.

"Ninasisitiza umuhimu wa wakazi kufuata taratibu sahihi za kuhamia Msomera. Serikali inahakikishia utoaji wa stahiki zote kwa mujibu wa sheria. Tumekutana na changamoto ambapo watu walihamia Msomera bila kufuata taratibu na baadaye wakakaa nyumba ambazo hazikutengwa rasmi," alisema Mbillu.

Alisisitiza kundi lililokuwa linaondoka kutoruhusu ndugu zao waliowaacha Ngorongoro kuhama bila kufuata utaratibu wa serikali ili na wao wapate stahiki zao kama ilivyokuwa kwao. Aliwahakikishia wakazi wanaohama kuwa serikali inafanya jitihada za kuboresha maisha yao kwa kutoa miundombinu wezeshi nje ya eneo la hifadhi na kuwa wanazingatia kanuni za sheria, kanuni na haki za binadamu.

Meneja Mradi anayesimamia Mpango wa Uhamaji wa Hiari, Ofisa Uhifadhi Mkuu, Florah Assey, alisema hadi kufikia Aprili mwaka huu, kaya 1,373 zenye watu 8,364 na mifugo 36,341, zimehamishwa ndani ya hifadhi hiyo tangu kuanzishwa kwa mpango wa uhamaji wa hiari Juni 2021.

Assey, alisema suala la uhamaji linaendelea vizuri, hamasa ya watu kuhama imekuwa ikiongezeka siku hadi siku kutokana na jitihada za kutoa elimu, kusajili na kutathmini mali za wakazi waliopo ndani ya hifadhi hiyo.

"Kila mkuu wa kaya iliyosajiliwa na wategemezi wake wanapatiwa nyumba ya vyumba vitatu vya kulala kwenye kiwanja cha ekari 2.5, shamba la ekari tano la kilimo na huduma muhimu za kijamii katika makazi yao mapya," alisema.

Kaimu Kamishna wa Uhifadhi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Victoria Shayo, alisema timu za usajili zimefika katika vijiji vyote vilivyopo ndani ya eneo la hifadhi.



Waandishi wa habari mkoani Shinyanga wakiwa kwenye ziara na Mamlaka ya Kudhibiti Huduma ya Nishati na Maji (EWURA) katika kituo cha uzalishaji maji ya Ziwa Victoria kilichoko Ihelele wilayani Misungwi, mkoani Mwanza juzi. Maji hayo hupelekwa Shinyanga na mikoa mingine jirani na sasa yamefika Shelui mkoani Singida. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wanavijiji 3,000 kufunzwa kumkabili simba

Na Elizabeth Zaya

ZAIDI ya wakazi 3,000 waishio vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti (SENAPA), wanatarajia kupatiwa elimu ya kukabiliana na wanyama wakali hususani simba ili kunusuru maisha yao.

Elimu ya kukabiliana na wanyama hao inatolewa kupitia filamu inayojulikana kama 'Kuishi na simba' iliyotengenezwa na msanii wa filamu nchini, Erica Rugabandana.

Filamu hiyo inalenga kufahamu hatari za kukabiliana na wanyama hao ambao hutoka hifadhini na kwenda kwenye makazi ya watu, ikimwangazia zaidi simba.

Pia, inasaidia kufahamu uhusiano wa mnyama huyo na binadamu, namna wanavyosambaa kwenye jamii na tabia zao, kulisha mifugo kwa wananchi wanaoishi karibu na hifadhi wanakohifadhiwa simba hao ili kuepuka hatari ya kushambuliwa.

Utafiti umebaini kuwa katika asilimia 40 ya simba pori waliosalia duniani, Tanzania ni kinara katika uhifadhi wa wanyama hao.

Kwa mujibu wa Rugabandana, filamu hiyo ni muhimu kwa jamii zinazoishi na wanyamapori si kwa Tanzania pekee bali Afrika Mashariki zikiwamo Kenya na Uganda ambako kumekuwa na matukio mengi ya simba kushambulia mifugo na binadamu.

"Ninaamini filamu hii itasaidia hata kuleta mijadala ya migogoro ambayo imekuwa ikitokea baina ya binadamu na wanyamapori, hivyo mamlaka husika nchini kuweka mikakati juu ya uhifadhi bora wa wanyamapori hao. Mijadala hiyo itasaidia kutoa taarifa za utungaji sera, programu za elimu na ushirikishwaji wa jamii katika masuala haya," alisema.

Alisema filamu hiyo imeanza kuonyeshwa kwenye shule na maeneo ya jamii zinazoishi karibu na mbuga za wanyama Kaskazini mwa Tanzania.

"Filamu hii imeonyeshwa kote duniani ikiwa ni pamoja na Tamasha la Filamu la Australia la Wild Earth Oceania mapema mwaka huu na itaonyeshwa katika Ubalozi wa Australia nchini Kenya mwezi ujao kama sehemu ya tamasha pekee la filamu za wanyamapori barani Afrika, yaani Pridelands Wildlife Film Festival," alisema.

# Maofisa mikopo wapigwa msasa kukopesha wakulima

Na Maulid Mmbaga

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) ikishirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), wamewapatia mafunzo maofisa mikopo 52 kutoka benki washirika 20 kwa lengo la kuwaongezea uelewa wa kutoa mikopo ya kilimo kwa wakulima nchini.

Vilevile, mafunzo hayo yanalenga pia kuzijengea uwezo taasisi za fedha ili kuziongezea maarifa na ujuzi kwa wataalamu wa fedha kwenye kilimo ili kuchagiza ongezeko la upatikanaji huduma za fedha, mikopo na rasilimali watu kwenye sekta za kilimo, mifugo na uvuvi nchini.

Akizungumza katika hafla ya kufunga mafunzo hayo, Kaimu Mkurugenzi wa TADB, Kaanaeli Nnko, alisema lengo la programu hiyo ni kuhakikisha wakulima wanafikiwa katika mikoa yote.

Nnko, alisema hadi sasa mfuko wao umedhamini mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 270 kupitia kwa benki washirika.


Alisema mikopo ya kilimo ni tofauti na ya kawaida, hivyo moja ya maeneo yaliyozingatiwa katika mafunzo hayo ni kuangalia namna gani ya kupunguza hatari ambayo itawawezesha watoa mikopo kubaini viashiria hatarishi na kuweza kuvizuia ili taasisi zisipate hasara.

"Hadi tunapozungumza tumeweza kufikia wakulima walengwa 24,000. Na tunaamini kwa haya mafunzo na washiriki tutakuwa na mafanikio zaidi, kwenye sekta ya kilimo hadi sasa benki washirika wametoa asilimia 11 ya mikopo na lengo letu ifikapo 2030 sekta ya mikopo yote inayotolewa itakuwa imefika asilimia 30," alisema Nnko.

Makamu Mkuu wa Chuo cha BoT, Dk. Ephraim Mwasanguti, alisema TADB iliwapatia jukumu la kutengeneza programu kwa ajili ya wakulima wadogo ikilenga kuwaelimisha maofisa mikopo wa benki washirika wanaosimamia skimu ya mikopo ya TADB ili watoe mikopo ambayo italipika.

Meneja Uhusiano Kilomo Biashara Benki ya CRDB, Salvatore Silvester, ambaye ni miongoni mwa walioshiriki mafunzo hayo, alisema programu hiyo imewasaidia kufungua mtazamo wao kukiangalia kilimo tofauti.

Mafunzo hayo kwa awamu ya kwanza yametolewa na wakufunzi kutoka BoT Academy, wataalamu kutoka Chuo cha Kilimo Sokoine (SUA) na Chuo cha Mtakatifu Agustino (SAUT) kuanzia Aprili 22 hadi Mei 3, mwaka huu.





Mwonekano wa baadhi ya nyumba zinazojengwa kwa ajili ya waathirika wa maafa yaliyotokea Wilaya ya Hanang mkoani Manyara, nyumba hizo zinajengwa eneo la Gidagamowd lililopo katika Kitongoji cha Waret wilayani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi ya uhujumu uchumi kunguruma leo

**Na Tumaini Mafie,**
ARUSHA

KESI ya uhujumu uchumi inayowakabili watumishi watatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na kuisababisha serikali hasara ya Sh.milioni 64.2, itaanza kutajwa leo katika Mahakama ya Wilaya ya Arusha mkoani hapa.

Washtakiwa hao wanaokabiliwa na mashtaka tisa ni Amani Mlay, Gerson Mollel na mmiliki wa Kampuni ya Usambazaji Vifaa vya Umeme na Mabomba, Cecy Zumba.

Kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu Mkazi, Devotha Msofe. Kwa mujibu wa Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Sifael Mshana, mshtakiwa wa kwanza (Mlay), anashtakiwa kwa matumizi mabaya ya nyaraka, kumdanganya mwajiri wake kuhusu dokezo lenye ombi la kiasi hicho cha Sh. milioni 64.2 zinahitajika kwa ajili ya vifaa vya umaliziaji wa ujenzi wa uzio wa Shule ya Msingi Shangarao iliyopo Kata ya Muivaro.

Katika maelezo ya kosa katika nyaraka hiyo ilikuwa ikionyesha Cecy Electrical Plumbing Co. Ltd, iliomba Sh. milioni 64.2.

Katika kosa la pili la matumizi ya nyaraka yenye maelezo ya uongo kutoka kwa Cecy, yakionyesha amewasilisha nyaraka yenye manunuzi ya nondo 500 zenye ukubwa milimita 12 na nondo 500 za milimita 8.

Manunuzi mengine ni malori saba ya kokoto, sita ya mchanga, mifuko 350 ya saruji, matofali 4,000 na wilbaro moja.

Kosa la tatu ni kumdanganya mwajiri wake kuwa Mei 25 mwaka jana kwa kutoa nyaraka ya uongo ya madai ya malipo, ikionyesha anadai Sh. milioni 64.2.

Kosa la nne, ni matumizi mabaya ya nyaraka yenye muhtasari wa kikao cha kamati ya usimamizi wa mradi wa umaliziaji wa ujenzi wa jengo hilo, huku akijua si kweli.

Kosa la tano, linamkabili Cecy Zumba kwa kusaidia kutenda uhalifu, ambapo anadaiwa kutenda kosa kati ya Mei 1 hadi Desemba mwa jana.

Kosa la sita, linamkabili Cecy na Mollel, kumsaidia Mlay kufanya uhalifu kwa kutumia nyaraka za uongo kwa ajili ya kumdanganya mwajiri wake kusaini zilizotokana na kikao.

Kosa la nane, ni wizi kwa watuhumiwa wote, kati ya Mei 1 hadi Desemba mwaka jana.

Vilevile, kosa la tisa linawakabili washtakiwa wote na kuisababishia mamlaka hasara.

# Wanakijiji waachana na maji ya makorongoni, madimbwi

**Na Godfrey Mushi,**
MANYARA

HATIMAYE zaidi ya wakazi 1,500 wa Kijiji cha Gadabagara kilichoko Wilaya ya Babati mkoani hapa wameondokana na adha ya zaidi ya miongo miwili kusaka maji kwenye makorongo, madimbwi na mapango kwa matumizi ya nyumbani baada ya kujengewa mradi wa maji.

Akizungumzia mradi huo jana, Meneja wa World Vision (WVT), Kanda ya Kaskazini, Juliana Charles, alisema ujenzi wa mradi wa maji umeigharimu kiasi cha Sh. milioni 291.669.

Juliana, alieleza hayo wakati wa hafla ya kukabidhi mradi huo, uliotekelezwa na WVT kwa kushirikiana na Wakala wa Maji Vijijini Wilaya ya Babati (RUWASA).

"Ili kuufanya mradi huu kuwa endelevu na kuwanufaisha vizazi kwa vizazi, tumeanza kutoa mafunzo kwa kamati ya maji ya kijiji, juu ya namna ya usimamizi na uendeshaji wa mradi huu," alisema Charles.

Alisema maji yaliyochimbwa yalipimwa na kuthibitishwa kuwa ni safi na salama na yanakubalika kwa matumizi ya binadamu.

Kwa mujibu wa Meneja huyo, mradi huo pia utawanufaisha wanafunzi 610 wa Shule ya Msingi Gidabagara.

Mkurugenzi wa World Vision Tanzania, Simon Moikani, alisema wao kama wahisani wanahitaji kuona miradi waliyoanzisha inakuwa endelevu baada ya kukamilika.

"RUWASA mnaweza mkatuma wataalamu Lake Eyasi (Ziwa Eyasi) wajifunze namna ya kutunza miradi ikawa endelevu, na mkawa mnakusanya fedha nyingi," alisema Mkurugenzi huyo.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga alionyesha kuridhishwa na ujenzi wa mradi huo unaozalisha lita za ujazo za maji 50,000 kwa siku.

Sendiga, alisema licha ya vitongoji vitatu kuanza kupata maji kupitia mradi huo, aliagiza RUWASA kusamba huduma hiyo kwenye vitongoji viwili vilivyobakia.

Alisema, pia vilula 10 vya kutoa huduma ya majisafi na salama vilivyopo katika kijiji hicho havikidhi mahitaji na kuiagiza RUWASA kuongeza vingine.

"Suala la upatikanaji wa maji, siyo la kubahatisha ni la kimkakati. Na wananchi kupata maji hawajafanyiwa hisani, ni haki yao ya msingi," alisisitiza Mkuu huyo wa Mkoa.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Gidabagara, Halima Shaban, alisema kabla ya kutekelezwa kwa mradi huo walikuwa wakitumia maji ya madimbwi yna kukumbwa na maradhi, ikiwamo ya kuhara.

Uchunguzi wa Nipashe umebaini kuwa kabla ya kujengwa kwa mradi huo, wanawake na watoto wa eneo hilo, walikuwa waathirika wakubwa wa kero hiyo, huku wanafunzi wakikatisha masomo, na wanawake wakishindwa kufanya shughuli za uzalishaji kutokana na kutumia muda mwingi kutafuta maji.

# Waendesha bodaboda 200 wanolewa

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya madereva bodaboda 200 wa Jiji la Arusha wamepatiwa mafunzo maalum ya usalama na afya kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kutambua vihatarishi vya ajali na magonjwa katika shughuli zao za uzalishaji.

Mafunzo hayo yaliyotolewa na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa ushirikiano na Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA), ni sehemu ya programu za kutoa elimu ya usalama na afya miongoni mwa makundi mbalimbali ya wajasiriamali wadogo ambayo imetolewa katika wiki ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

Akitoa mafunzo hayo kwa madereva hao, Meneja Mwandamizi wa Afya, Usalama na Mazingira kutoka GGML, Dk. Kiva Mvungi aliwasihi madereva hao kujiepusha na ajali zinazozuilika kwa kuheshimu alama pamoja na barabarani.

Alitoa wito kwa madereva hao kujenga tabia ya kupima afya mara kwa mara ikiwamo magonjwa yasiyoambukiza kama vile kisukari, presha na moyo ili kufanya kazi hiyo kwa utulivu.

"Lakini sio kila namba unayopewa na mdada unaisave, watawachukulia hela zenu zote. Jifunzeni kuhifadhi fedha ili baada ya muda uwe na bodaboda yako binafsi au uongeze nyingine na hata kufungua biashara mbalimbali," alisema.

Ofisa Usimamizi wa Afya na Usalama mahali pa Kazi kutoka GGML, Kulwa Simba, alisema mafunzo hayo yalilenga kuwasaidia madereva hao namna ya kutambua na kujikinga ili kutoingia kwenye ajali zisizo za lazima.

"Pia tumewafundisha namna ya kuokoa mtu aliyepata ajali ya bodaboda kwa sababu ilikuwa ni utamaduni kwamba ajali ni sehemu ya maisha yao. Lakini tumewasisitiza kwamba dereva mmoja ana familia, ndugu na jamaa wanaomtegemea hivyo ni vema kuwa makini.

Kulwa aliongeza kuwa GGML iliwagawia washiriki hao baadhi ya vifaa kinga yakiwamo mavazi yanayomtambulisha mtu akiwa katika eneo la kazi 300.

Awali akifunga mafunzo hayo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Deogratius Ndejembi, aliwapongeza washiriki kwa kutambua umuhimu wa mafunzo hayo na kujitokeza kwa wingi na kuwataka kutumia ipasavyo maarifa waliyoyapata kuboresha kazi yao ya usafirishaji.

"Baada ya mafunzo haya sitarajii kuona mtu yoyote miongoni mwenu anakuwa sehemu ya waendesha pikipiki wanaovunja sheria za barabarani ikiwamo kuvipita vyombo vingine vya moto bila kuwa na tahadhari yoyote. Niwahakikishie kuwa serikali yenu chini ya Rais wetu Samia Suluhu Hassan, inawathamini na itaendelea kuwapa mafunzo pamoja na fursa za mitaji ili muweze kujiinua kiuchumi," alisema.

Akimkaribisha Waziri kufunga mafunzo hayo, Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, aliwapongeza washiriki wa mafunzo hayo kwa kujitoa na kutenga muda wao ambao wangeutumia kufanya shughuli zao za uzalishaji.

Akitoa shukrani kwa niaba ya washiriki wenzake, Mwenyekiti wa Umoja wa Bodaboda Wilaya ya Arusha, Okelo Costantine, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwapigania vijana kufanya kazi zao kwa utulivu na kuwapatia fursa ikiwamo za mafunzo.

Mafunzo hayo ambayo yamefanyika Aprili 29, mwaka huu katika Uwanja wa General Tyre uliopo Njiro, yalijumuisha mada mbalimbali zikiwemo utambuzi wa vihatarishi vya usalama na afya katika shughuli za usafirishaji na utoaji wa huduma ya kwanza kwa waathirika wa ajali za barabarani.







Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi (katikati), akikata utepe kuashiria ufunguzi wa jengo la Dawati la Jinsia la Wilaya ya Nyamagana, lililojengwa na Shirika la SOS Children's Villages na wadau mbalimbali lililogharimu Sh. milioni 66.5, katika warsha hiyo Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, DCP Wilbrod Mutafungwa, alibainisha kuanzia mwaka 2022 hadi Aprili 2024 matukio ya ubakaji yalikuwa 537, mimba kwa wanafunzi 534 na ulawiti 197. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Waume wadaiwa kushushia vipigo wenza, kuwapora mikopo

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

BAADHI ya wajasiriamali wanawake wa Kata ya Mwamala wamedai hawanufaiki na mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kutokana na kuambulia vipigo na kuporwa na waume zao na kushindwa kurejesha.

Madai hayo waliyatoa wiki iliyopita wakati wakizungumza na Nipashe kuhusu utekelezaji wa mradi wa wanajamii na vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto unaofadhiliwa na Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Mwenyekiti wa Kikundi cha Vumilia, Ester Mandi, alisema pamoja na serikali kuwa na lengo la kuwainua kiuchumi kwa kupatia fedha mikopo isiyokuwa na riba ili kukuza mitaji yao, wanapogawana kwa lengo la kuwekeza katika biashara, wananyang'anywa na waume zao na kushindwa kurejesha.

Alisema ili kudhibiti tatizo hilo ni vyema serikali iwaelimishe wanaume ili watambue mikopo inayotolewa kuwaendeleza wanawake na vijana.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Mkombozi, Anna Nkinga, alisema walikopeshwa Sh.milioni 4 kwa ajili ya kuanzisha mradi wa ufugaji ng'ombe, lakini wameingiliwa na waume zao kwa madai mwanamke hawezi kufanyabiashara wakati mwanaume yupo na kusimamia wao.

"Mkopo huu tumefanikiwa kuulipa wote na kikundi chetu hakidaiwi, lakini marejesho yake ilikuwa ni kuvutana mpaka Ofisa Maendeleo wa Jamii alipoingilia kati tena kwa kuwaita waume zetu kwa barua na kuwalazimisha kulipa," alisema Nkinga.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Mwamala, Sophia Philbert alithibitisha baadhi ya vikundi vya ujasiriamali vilivyopokea mikopo hiyo kushindwa kurejesha.

Hata hivyo, Sophia, alisema ofisi yake itahakikisha vikundi hivyo vinarejesha mikopo hiyo ili kuvipatia fursa vingine kunufaika na fedha hizo za serikali.

Alisema baadhi ya wanaume wamekuwa wakifika ofisini kwake kuilalamikia serikali kwa kuwapatia mikopo hiyo wanawake na vijana na kuwaacha wao wakati wana uwezo wa kufanya biashara.

Alisema ofisi yake imebaini kuna wanaume wamebuni mbinu ya kuwatumia wanawake kuunda vikundi, kuwakopea fedha na kuwakabidhi jambo ambalo ni kinyume na sheria.

# Hama hama ya wafugaji yaachisha shule wanafunzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TABIA ya baadhi ya wafugaji wa Kijiji cha Ng'homango wilayani hapa kufuata malisho inadaiwa kusababisha wanafunzi kuacha shule na kushindwa kutimiza ndoto ya kupata elimu.

Hayo yalisemwa juzi na Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Ng'homango, Peter Yuga wakati akizungumza juzi na Nipashe shuleni hapo kuhusiana na tatizo hilo.

Yuga, alisema hali ya uhamaji kijijini hapo ni kubwa huku wanafunzi wakiachishwa masomo bila kujali hata wale waliopo kwenye madarasa ya mtihani.

"Mwaka jana tulifanikiwa kumtafuta kwa ushirikiano na viongozi wa serikali na kumrejesha mwanafunzi wa darasa la nne ili afanye mitihani na kuendelea na masomo baada ya kutoroshwa," alisema Yuga.

Alitoa wito kwa wazazi ambao ni wafugaji wanapotaka kuhama kwenda kutafuta malisho mikoa mingine, waangalie uwezekano wa kuacha familia zao ili watoto waendelee na masomo hasa wa madarasa ya mtihani ili waweze kutimiza ndoto zao.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ng'homango, Madilya Nyema, alisema mwaka jana hali ilikuwa mbaya zaidi kutokana na wafugaji kuhamishwa katika eneo la Hifadhi ya Msitu wa Nindo.

Nyema, alisema serikali na walimu wamekuwa wakishirikiana kudhibiti wanafunzi kuachishwa shule ili waendelee kupata elimu kwa kuwa ni haki yao ya msingi.

# FAO yataka wadau kudhibiti magonjwa ya mlipuko nchini

**Na Rose Jacob,** MWANZA

SHIRIKA la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) limewataka wadau nchini kushirikiana elimu juu ya dhana ya Afya Moja kwa jamii ili kukabiliana na magonjwa ya mlipuko nchini.

Rai hiyo ilitolewa juzi jijini hapa na Mratibu wa Mradi wa Kudhibiti Usugu wa Vimelea vya Magonjwa dhidi ya Dawa wa FAO, Dk. Elibariki Mwakapeje wakati wa kikao kazi na wadau wa sekta ya afya.

"Tumewajengea uwezo viongozi wa ngazi za wilaya, halmashauri za Mkoa wa Mwanza dhidi ya Afya Moja. Suala hili tunalipa kipaumbele kwani kuna maradhi na matatizo wanayowapata binadamu kutokana na vyakula husani vitokanavyo na mimea na mifugo ambavyo vimekuwa na matumizi makubwa ya dawa," alisema Dk. Mwakapeje.

Aliwataka wadau hao kutumia njia tofauti katika kuielimisha jamii ili kukabiliana na athari zitokanazo na magonjwa hayo.

Mkurugenzi Msaidizi wa Afya Moja Ofisi ya Waziri Mkuu, Dk.Saluum Manyata, alisema kuwa asilimia 60 ya magonjwa yatokanayo na wanyama yanawakumba binadamu.

Dk. Manyata, alisema asilimia 75 ni magonjwa mapya, hali iliyoifanya serikali kukaa pamoja na wadau kuhakikisha wanatatua kupitia sekta ya afya, kilimo na wanyama.

Akifungua kikao hicho, Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Christopher Emily Ngubiagai, alisema dhana hiyo inalenga kuimarisha ushirikiano wa kisekta, kupambana na matatizo mtambuka

# Ubakaji, mimba kwa wanafunzi vyatikisa Mwanza

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MATUKIO ya ubakaji, ulawiti na mimba kwa wanafunzi yanaongoza mkoani hapa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2022 hadi Aprili 2024. Takwimu hizo zilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbrod Mutafungwa wakati wa uzinduzi wa jengo la Dawati la Jinsia la Wilaya ya Nyamagana, lililojengwa na Shirika la SOS Children's Villages kwa gharama ya Sh. milioni 66.5.

Mutafungwa alisema kuwa takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi hicho, matukio ya ubakaji yanaongoza kuwa 537, yakifuatiwa na mimba kwa wanafunzi 534 na ulawiti 197.

Alisema licha ya serikali kuendelea kupambana kudhibiti vitendo hivyo, bado vimeendelea kukithiri na watuhumiwa kuendelea kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

"Tangu kuanzishwa madawati ya jinsia mwitikio wa wananchi kutoa taarifa za ukatili na uhalifu umeongezeka na matukio kwa sasa hayafichwi, hatua zinachukuliwa dhidi ya watuhumiwa," alisema. Akizungumzia kuhusu watoto kutelekezwa na wazazi na walezi wao, alisema kwa kipindi hicho matukio 131 yaliripotiwa, wanafunzi kutoroshwa 69, watoto kutupwa 43, kuibwa 35 na kujamiiana na ndugu zao 16.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina, Makilagi alilipongeza shirika hilo kwa kujenga jengo hilo na kuwataka wadau wengine kuiga mfano huo.

Makilagi, aliwataka wananchi kutoa ushahidi mahakamani dhidi ya watuhumiwa ili wachukuliwe hatua na kuwafichua wanaojihusisha na vitendo hivyo ili vitokomezwe katika maeneo yao.

Mratibu wa Mpango wa kuimarisha familia wa SOS Children's Villages, Elizabeth Swai, alisema wanawake na watoto wanaofanyiwa ukatili watahudumiwa kwa usiri na kubaki salama huku watuhumiwa wakichukuliwa hatua. "SOS Children's Villages tunatoa elimu kwa jamii ili kuimarisha ulinzi wa watoto na kuhakikisha usalama wao unakuwepo ngazi ya kaya hadi katika jamii na kuhakikisha taarifa za ukatili zinazoibuliwa zinashughulikiwa," alisema na kuongeza: " Tumechangia ujenzi huu, tumenunua vitanda na magodoro."

Alisema wanashirikiana na serikali kupinga ukatili wa kijinsia katika jamii, hivyo ni wakati wao wa kuendelea kutoa dhidi vya vitendo hivyo bila woga.

Nipashe
Spotika



VIUNGO WAKABAJI 15 BORA KWA SASA DUNIANI UK. 12

# VAZQUEZ, NACHO NA MICHEZO 700, MATAJI 39 MAGWIJI WASIOIMBWA



Luca Modric Nacho Vazquez

**MADRID, Hispania**

WAMEUNGANISHWA kwa jumla ya mechi 700 na mataji 39 kwa Real Madrid, lakini Lucas Vazquez na Nacho bado wanaruka chini ya rada, wakiwa na wasifu wa chini sana kuliko wenzao wanaoshereheka.

Katika wiki za hivi karibuni, hata hivyo, wakongwe hao wa muda mrefu wametoka kwenye kivuli na kuchukua majukumu muhimu katika timu yao.

**LABDA ILIKUWA WIKI BORA ZAIDI YA KAZI YA VAZQUEZ.**

Baada ya kutoka kwenye benchi wakati wa mkondo wa pili wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya huko Manchester City, akichukua nafasi ya Vinicius Junior wakati wa muda wa ziada, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, alipewa jukumu la kupiga penalti ya tatu ya timu yake na wakatinga nusu fainali.

Vazquez aling'ara zaidi siku nne baadaye Real ilipoikaribisha Barcelona kwenye El Clasico.

Akiwa nafasi ya Dani Carvajal katika nafasi ya beki wa kulia, alishinda penalti kwa bao la kwanza la timu yake, akafunga la pili kwa umaliziaji mzuri mara ya kwanza na kufanya 2-2 na kisha kufanya kazi nzuri kwa kutoa krosi kwa Jude Bellingham aliyefunga bao la ushindi.

Mchezaji huyo wa England alionesha shukrani zake kwa kujiunga na Vazquez kwa mchezo wa kusherehekea na baadaye akachapisha ujumbe mfupi wa mtandao wa kijamii: Lucas Vazquez wewe ni gwiji.

Maelezo hayo si ya kutia chumvi sana, kwa sababu katika muongo mzima uliopita kuwapo kwa Vazquez kwa uthabiti chini ya ubavu wa kulia - ama kama winga wa jadi au beki wa pembeni mbabe - kumekuwa sifa thabiti ya timu inayoendelea kubadilika.

Mzaliwa wa Kaskazini-Magharibi mwa eneo la Hispania la Galicia, Vazquez alihamia mji mkuu na kujiunga na Real akiwa na umri wa miaka 16. Baada ya kufanikiwa kupitia safu ya vijana ya klabu hiyo, alipandishwa ngazi hadi kwenye kikosi cha wakubwa kwa mkopo wa msimu mzima huko Espanyol mnamo 2014-15.

Mara moja alionesha kuwa mchezaji asiyechoka ambaye alichanganya maadili ya timu na matokeo ya kushambulia, alicheza mechi 39 wakati wa kampeni hiyo ya kwanza na alipandishwa kwenye kikosi cha wakubwa cha Real aliporejea.

Tangu wakati huo hajawahi kuwa mbali na hatua hiyo, akicheza angalau mechi 30 kila msimu isipokuwa 2019-20, ambapo alikosa baada ya kuvunjika kidole.

Mbele ya nyota kama vile Gareth Bale, Rodrygo na Carvajal upande wa kulia, Vazquez amekuwa akianza mara Kwa mara. Lakini daima amekuwa tayari kungoja kwa subira zamu yake.

Vazquez anaweza kuwapo kwa muda mrefu zaidi - ingawa mkataba wake unamalizika msimu huu wa majira ya joto, anafikiriwa kuwa karibu kukubaliana na mkataba mpya wa kuongeza muda wake wa kukaa hapo Bernabeu.

Mfungaji mwingine wa penalti aliyefanikiwa katika mkwaju wa penalti dhidi ya City alikuwa Nacho, ambaye alicheza dakika zote 120 kwenye eneo la ulinzi na kufunga mkwaju wa nne kwa kumpeleka maboya Ederson.

Hapo awali alikuwa ametoa uchezaji bora kumzuia Erling Haaland, na jukumu lake kuu katika ushindi dhidi ya mabingwa hao wa England.

Mejeraha ya muda mrefu kwa Eder Militao na David Alaba yamemfanya Nacho kuungana na Antonio Rudiger katika safu ya ulinzi ya kati ya Carlo Ancelotti.

Imani ya Ancelotti kwa Nacho ilisisitizwa mnamo Januari wakati klabu ilikataa kukimbilia soko la uhamisho licha ya majeraha ya Militao na Alaba, badala yake waliweka imani yao kwa Nacho kuongeza kasi.

Na hilo sio jambo jipya, kwa sababu kocha huyo wa Italia amekuwa mtetezi wa hali ya juu wa uwezo mbalimbali wa Nacho, ambaye aliteuliwa kuwa nahodha wa klabu kutokana na kuondoka kwa Karim Benzema majira ya joto yaliyopita.

Hasa, Ancelotti amempa sifa za kipekee za kuwa beki "asiye kata tamaa" - kila wakati akitarajia mazuri zaidi kutokea, na kwa hivyo kuwa na matarajio muhimu ya kuzima nyakati za hatari ambazo wengine hawangetarajia.

**NACHO AMEKUWA SEHEMU YA REAL MADRID TANGU 2001**

Mafanikio ya Nacho katika kutengeneza taaluma ya kung'ara ni ya kuvutia zaidi kwa kuwa aligunduliwa kuwa na kisukari akiwa na umri wa miaka 12, mwaka mmoja baada ya kujiunga na kikosi cha vijana cha Real.

Alipuuza ushauri wa awali wa kuacha kucheza soka na sasa anakiri ugonjwa wa kisukari kwa kusaidia kazi yake kukua, na kumlazimu kujifunza katika umri mdogo kuwajibika kwa mwili wake na lishe yake.

Hisia hiyo ya kujitegemea imekuwa ikidhihirika kila mara katika uchezaji wake, huku Nacho akizunguka bila kulalamika pengo lipi la nyuma linalohitaji kujazwa, mara nyingi akisubiri kwenye benchi bila kulalamika.

Onesho lake dhidi ya City huenda lisitoshe kumuweka kwenye timu. Militao sasa yuko fiti tena na anaweza kumtoa Nacho kwa nafasi ya pili.

Kama Vazquez, Nacho mwenye umri wa miaka 34, pia mkataba wake unamalizika msimu huu wa majira ya joto, lakini kuna uwezekano mdogo wa kurejea tena huku kukiwa na uvumi unaomhusisha na kuhamia Italia na Marekani.

Baada ya zaidi ya miaka 20 kwenye vitabu vya Real itakuwa vigumu kusema kwa heri, lakini kunyanyua Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya litakuwa jambo zuri zaidi kwake.

## ISIKUPITE

HII ni mara ya kwanza kwa Erling Haaland, kufunga mabao manne kwenye mechi moja ya Ligi Kuu England, baada ya kufanya hivyo juzi wakati Manchester City ikishinda 5-1 dhidi ya Wolves. Hata hivyo Haaland ameshafunga mabao matano mara mbili katika mechi ya Kombe la FA dhidi ya Luton na pia dhidi ya RB Leipzig Machi mwaka jana kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwa sasa amefikisha jumla ya hat-tricks tisa katika ligi hiyo tangu ajiunge na Man City.



## Extra Time

# VIUNGO WAKABAJI 15 BORA KWA SASA DUNIANI


RODRI

**LONDON, England**

KATIKA mchezo wa soka wa kisasa, kiungo mkabaji anatakiwa kuwa katika kiwango bora kwa muda wa dakika 90, akikimbia huku injini yake ikiwa na kasi kamili.

Wanahitaji kuwa wakandamizaji wasiochoka, wanaoweza kusoma kila hali inayoweza kuwaziwa lakini pia kuwa na kipaji kwenye mpira, wenye uwezo wa kuupapasa kwa ustadi karibu na eneo la karibu au kuokota pasi ya mbali. Mara nyingi, ni vigumu kupata kutambuliwa katika pande bora duniani, lakini kila timu kubwa mara nyingi huwa na namba sita inayofanya mambo kuwa sawa.

Makala haya yanawachambua viungo wakabaji 15 ambao ni kinara wa mchezo kwa sasa - kimsingi kulingana na uchezaji wa sasa na msimamo wa kiwango cha juu, kwa kuzingatia majeraha na kuwatenga wale ambao ni wa kawaida, twende sasa...

**15. Andre-Frank Zambo Anguissa**

Kila kitu kilienda sawa kwa Napoli wakati wa msimu wao wa 2022/23 wa kushinda taji la Serie A.

Safu ya kiungo ya Luciano Spalletti ilikuwa na uzani wa kutosha, huku Andre-Frank Zambo Anguissa - ambaye zamani alikuwa Fulham - akisawazisha kikamilifu mchango wa ulinzi na ukimbiaji wa mbele wa akili.

Kama wengine wote huko Napoli, msimu huu amekuwa na shida chini ya Rudi Garcia na Walter Mazzarri.

**14. Edson Alvarez**

Edson Alvarez amekuwa bora zaidi kwa West Ham msimu huu na amesaidia kupunguza athari za Declan Rice kuihama klabu hiyo.

Mkurugenzi wa ufundi wa West Ham, Tim Steidten amemsifu Alvarez kama "muhimu sana," akirejea maoni mazuri yaliyotolewa na kocha David Moyes.

**13. Manuel Ugarte**

Paris Saint-Germain ilishinda mbio za kumsajili Manuel Ugarte wakati wa majira ya joto na ni usajili ambao umeweza kuleta mabadiliko makubwa kwa safu ya kiungo ya klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ni mmoja wa washindi bora wa mpira kote. Hajatawala Ligue 1 jinsi PSG wangeweza kutarajia hadi sasa, lakini alikuwa usajili mzuri.

**12. Casemiro**

Casemiro ni mmoja wa viungo wa kisasa wa ulinzi, akiwa ameshinda mataji mengi kama mtekelezaji mkuu wa Real Madrid miaka ya 2010.

Tamaa ya kujaribu kitu tofauti ilimfanya Mbrazil huyo ajiunge na Manchester United na alifurahia kampeni kubwa ya kwanza Old Trafford - wakati wowote hakutengwa kwa kusimamishwa.

Miguu ya Casemiro inayougua haimruhusu kukagua safu yake ya ulinzi ipasavyo na ameathiriwa na baadhi ya mbinu za Erik ten Hag, lakini anamiliki mpira vizuri na anabaki kuwa kiongozi muhimu wa Man Utd.

**11. Boubacar Kamara**

Boubacar Kamara alipewa kiwango cha juu sana katika klabu ya Marseille kwa muda mrefu, lakini aliishia kwenda chini ya rada kabla ya kusaini Aston Villa.

Chini ya Unai Emery, amekuwa mchezaji muhimu na anaweza kutajwa kwa kiasi kikubwa kutokana na nafasi yao nzuri ya ligi.

**10. Wataru Endo**

Usajili usio wa kawaida kwa Liverpool, Wataru Endo ameonekana kuwa mchezaji mwenye akili ukizingatia jinsi Wekundu hao walivyokuwa wepesi kwa viungo wa ulinzi.

Kama Jurgen Klopp alivyomwambia mchezaji huyo wa Kimataifa wa Japan alipowasili: "Tunakuhitaji sana. Tuna timu nzuri sana."

**9. Joao Palhinha**

Mchezaji anayecheza safu ya juu katika Ligi Kuu England msimu uliopita, ni sawa kusema Fulham hawakuweza kukaa bila Joao Palhinha.

Uhamisho wa majira ya kiangazi kuelekea Bayern Munich ulishindikana na Marco Silva bila shaka amekuwa mnufaika, huku kiungo huyo wa Ureno akitengeneza msimu mwingine mzuri hapo Craven Cottage.

**8. Douglas Luiz**

Kiungo wa kati wa Brazil, Douglas Luiz bila shaka ndiye mtu muhimu katika kikosi cha Unai Emery cha Aston Villa.

Uwezo wake ndani na nje ya mpira huwawezesha wachezaji walio mbele yake kwenda na kushinda michezo. Luiz pia ana jicho lililokuzwa zaidi la kufunga kuliko wenzake wengi wa safu ya ulinzi.

**7. Yves Bissouma**

Nyota wa zamani wa Brighton, Yves Bissouma alichukuliwa kama mchezaji bora aliyesajiliwa na Spurs wakati wa dirisha ambalo lilikusudiwa kuwavusha kwenye ulimwengu mpya huku Antonio Conte akisimamia.

Hata hivyo, msimu wa kwanza wa kiungo huyo hapo Kaskazini mwa London ulikuwa mgumu. Mechi zake chache za kwanza chini ya Conte hazikuwa za kiwango na ilionekana kana kwamba hakuwahi kuaminiwa na Muitaliano huyo kabla ya kuumia kwake.

Lakini kipaji cha Bissouma hakiwezi kubezwa na tumeona jinsi anaweza kuwa mzuri msimu huu chini ya kocha mpya, Ange Postecoglou.

**6. Granit Xhaka**

Uhusiano wa kiungo huyo na mashabiki wa Arsenal ulitiwa doa Oktoba 2019 alipokejeliwa na mashabiki alipokuwa akitoka nje ya uwanja. Wengi waliamini kuwa hilo halikuwa jambo la maana, lakini Xhaka aliendа haraka kurejesha heshima yake akiwa na 'Washikabunduki' hao.

Kuwasili kwa Mikel Arteta kulimpa mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswisi maisha mapya na akaibuka tena kama mtu muhimu Kaskazini mwa London. Wakati bado kulikuwa na wakati usio wa kawaida wa wazimu, Xhaka alijidhihirisha kama mtu wa chuma wa Arteta na mabadiliko ya jukumu mnamo 2022/23 yalisababisha msimu wake wenye tija zaidi katika rangi za Arsenal. Sasa yuko katikati ya kikosi cha Bayer Leverkusen na ametoa mchango mkubwa kukiwezesha kubeba ubingwa wa Bundesliga.

**5. Alexis Mac Allister**

Alexis Mac Allister alikuwa kiungo wa kati wa Brighton na Hove Albion wa 'box-to-box', lakini amechukua jukumu la kushikilia tangu ajiunge na Liverpool.

Amekuwa mzuri katika nafasi hiyo ya kina, hata kama nyakati zake za kuvutia zaidi zinaonesha kuwa mshindi wa Kombe la Dunia atashiriki mara kwa mara zaidi Anfield siku zijazo.

**4. Joshua Kimmich**

Joshua Kimmich ni mmoja wa wachezaji wa kiwango cha juu wanaoweza kubadilika zaidi katika mchezo wa leo na amekuwa katikati ya Bayern Munich kushinda mataji mara kwa mara katika miaka ya hivi karibuni.

Uzuri wake katika safu ya kiungo, uwezo wa kuweka mambo sawa na kuvunja uchezaji kwa kiwango ambacho hakijawahi kushuhudiwa humfanya kuwa mtaji bora, ambaye pia anaweza kucheza beki wa kulia inapohitajika.

**3. Aurelien Tchouameni**

Real Madrid ilimchunguza sana Aurelien Tchouameni wakati alipokuwa Monaco na lazima walifurahishwa na kazi kubwa ya ulinzi - hasa kukaba, ingawa mchezo wake unaoendelea sio mbaya pia.

**2. Rice Declan**

Declan Rice ameimarika kwa kiwango cha ajabu katika miaka ya hivi karibuni na sasa anaongoza safu ya kiungo ya Arsenal.

Wachezaji wachache wanaweza kufikia kiwango cha hali ya juu cha mchezaji huyo wa Kimataifa wa England wakati yeye pia amekuwa na nguvu kwenye upande mwingine wa uwanja katika kushambulia.

**1. Rodri**

Ilichukua msimu au zaidi kwa Rodri kupata nguvu ya soka ya Ligi Kuu England, lakini tangu kuzoea kumekuwa na wachache bora katika safu ya ulinzi kuliko Mhispania huyo.

Kwa haraka sana Rodri ameinua mchezo wake hadi kiwango cha juu zaidi, akionesha darasa lake na kurithi kiti cha enzi cha Fernandinho.

Kufunga bao la ushindi katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya pia kuliongeza hisa zake, lakini hata hivyo, Rodri ndiye bora katika nafasi yake kwa hivi sasa.

## Nukuu


"Nadhani katika kila kitu nilichofanya hapa kwa miaka minne, nilijitolea kila wakati. Lakini, kwa bahati mbaya, kila kitu kina mwanzo, katikati na mwisho. Hiyo haimaanishi kuwa huu ni mwisho wa uhakika. Natamani kuondoka, mlango ufunguke ili siku za usoni nirudi, japo kwa nafasi nyingine hapa lakini ni upendo usioelezeka. Tayari ni vigumu kusema kwa heri katika hali ya kawaida, lakini kunapokuwa na upendo wa pande zote, ni ngumu zaidi,**" Thiago Silva, akithibitisha uamuzi wake sasa wa kuondoka Chelsea.**



"Gabriel Jesus anataka kubaki Arsenal, lakini klabu bado inavutiwa kwenda sokoni katika dirisha la majira ya joto, kama tulivyoeleza mara nyingi. Hawataki usumbufu wowote sasa katika mbio za ubingwa, lakini Juni mtazamo wao wote ni suala la uhamisho akiwamo straika, hakuna kilichobadilika katika mipango ya Arsenal kwa sasa," **anaandika mwandishi nguli wa habari za michezo Ulaya, Fabrizio Romano.**



"Nadhani wote wawili ni wa kushangaza. Tunazungumza juu ya wachezaji wawili bora, sio tu ulimwenguni lakini historia ya mchezo huu. Siku zote nilisema Messi ana kipaji ambacho hakuna mtu anacho. Cristiano Ronaldo ni mchezaji tofauti sana, wanatofautiana sana [na Lionel Messi], ni mrefu, ana nguvu, amekamilika kweli kweli. Anaweza kufanya lolote. Anaweza kufunga magoli kwa kichwa, free-kick, penalti, moja kwa moja. Kwangu mimi, ni kama Messi si binadamu, lakini Cristiano ni binadamu bora zaidi,**" Beki wa zamani wa Barcelona, Gerard Pique, kuhusu mjadala wa nani bora kati Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.**



# WACHEZAJI WATANO WENYE REKODI ZA KUTAKATA LIGI KUU

Na Adam Fungamwangwo

ZIMESALIA raundi tano tu kuhitimisha msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2023/14, huku timu zikiwa zimeshajipambanua zenyewe kwenye msimamo.

Kuna zinazoonekana kusaka ubingwa, lakini kupata nafasi mbili za juu ili kucheza Ligi ya Mabingwa msimu ujao. Timu hizo ni Yanga, Simba na Azam FC ambazo moja wapo ndiyo itatwaa ubingwa, na mbili kati ya hizo zitacheza michuano hiyo ya kimataifa.

Zipo zinazowania nafasi ya nne, ili kujiwekea akiba ya kucheza Kombe la Shirikisho msimu ujao kutokana na kanuni zilivyo.

Timu itakayochukua ubingwa wa Kombe la FA, kama itakuwa ni moja kati ya timu tatu zitakazomaliza nafasi ya juu, basi itakayoshika nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu, nayo itacheza Kombe la Shirikisho.

Coastal Union, KMC na Prisons zinaonekana kuinyemelea nafasi hiyo msimu huu.

Hali ni mbaya kwa timu za Mtibwa Sugar inayoshika mkia, Tabora United, Mashujaa FC, Geita Gold, Ihefu na Namungo, ambazo kama hazikufanya vema katika michezo yao iliyosalia, ama zinaweza kushuka daraja, au kwenda kucheza mechi za mchujo na timu kutoka Ligi ya Championship.

Ukiacha matokeo na rekodi za timu, wachezaji nao wanapambana kila mmoja kujitengenezea rekodi yake.

Katika makala haya, tumekusanya takwimu za baadhi ya wachezaji wanaoonekana 'kuupiga mwingi' mpaka sasa ambao wanaweza kujiwekea rekodi binafsi mwishoni mwa msimu...




Kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto', akishangilia moja ya mabao yake aliyofunga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara inayoelekea ukingoni.

**1# Stephane Aziz Ki (mashuti ya mbali)**

Kiungo mshambuliaji huyu wa Yanga, anaongoza kwa kufunga mabao kwa mashuti ya mbali. Mburkina Faso huyo amefunga mabao matano akiwa nje ya boksi mpaka sasa. Aziz Ki, ambaye ndiye kinara wa mabao kwenye Ligi Kuu akipachika 15 kabla ya mechi ya jana, ni mmoja wa wachezaji ambao ni hatari kwa kupiga mashuti ya mbali, akiwa anakokota mpira, au kwenye mikwaju ya faulo.

Wakati Aziz Ki, aliongoza kwa mabao ya mashuti ya mbali, kiungo mshambuliaji mwingine wa Ihefu FC, Feisal Salum 'Fei Toto', yeye anaongoza kwa kufunga mabao ndani ya eneo la hatari. Feisal, maarufu kama Fei Toto, amefunga mabao 13 akiwa kwenye boksi.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa msimu huu akitokea Yanga, ana mabao 14 ya kufunga mpaka sasa, akishika nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji bora, nyuma ya Aziz Ki, hivyo inaonyesha kuwa ni bao moja tu alilolifunga akiwa nje ya boksi.

Wanaoshika nafasi ya pili kwa kupachika mabao ndani ya boksi ni kiungo mshambuliaji raia wa Burkina Faso, Stephane Aziz Ki wa Yanga na straika wa KMC, Waziri Junior, ambao wote wamefunga mabao 10 wakiwa ndani ya eneo la hatari.

**3# Mudathir (mfungaji bao la mapema)**

Kiungo mkabaji wa Yanga, Mudathir Yahaya, ndiye mfungaji wa bao la mapema zaidi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi kufikia raundi ya 25.

Bao alilofunga sekunde ya 48 dhidi ya KMC, Februari 17, mwaka huu, katika mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu linaendelea kuwa bao la mapema zaidi katika ligi mpaka sasa.

Katika mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa CM Kirumba jijini Mwanza, Yanga ilishinda mabao 3-0, mchezaji huyo akifunga mabao mawili, moja likifungwa na Pacome Zouzoua.

Anayeshika nafasi ya pili kwa kupachika bao la mapema ni kiungo mkabaji wa Azam FC, Sospeter Bajana, ambaye alifunga dakika ya 54, katika mechi ambayo timu hiyo ilicheza dhidi ya JKT Tanzania.

**4# Djigui Diarra (mbabe wa 'clean sheets')**

Kipa wa Yanga, Djigui Diarra, anaongoza kwa kukaa langoni mechi nyingi bila kuruhusu wavu wake kuguswa. Raia huyo wa Mali, amefanya hivyo mara 11, akifuatiwa na kipa wa Coastal Union raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Ley Matampi, aliye na 'clean sheets' 10 mpaka sasa.

Mechi iliyoamua nani awe juu katika makipa hao wawili, ilikuwa ni ya Aprili 27, kati ya Yanga dhidi ya Coastal Union, iliyochezwa, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Kabla ya mechi hiyo, kila mmoja akiwa na 'clean sheets' 10, lakini dakika 90 zilimalizika kwa Yanga kushinda bao 1-0.

**5# Kipre Junior (mkali wa 'asisti')**

Winga wa Azam FC, Kipre Junior, yuko juu ya watoa pasi za mwisho kwenye Ligi Kuu, akiwa amefanya hivyo mara nane mpaka sasa.

Raia huyo wa Ivory Coast mwenye 'asisti' nane, anafuatiwa na raia mwenzake na huko, Yao Kouassi, anayeichezea Yanga, pamoja na Mburkina Faso wa Yanga, Aziz Ki, ambao wote wana 'asisti' saba kila mmoja, huku Fei Toto akiwa nazo sita.

Wachezaji Awesu Awesu na Rahim Shomari wa KMC, Paschal Msindo na Lusajo Mwaikenda wa Azam FC, Clement Mzize wa Yanga, Clatous Chama wa Simba, na Impiri Mbombo wa Tabora United, wote wakiwa na 'asisti' tano kila mmoja.

## JE, WAJUA?



KIPIGO cha mabao 4-2 ilichokipata Barcelona dhidi ya Girona kinaifanya Real Madrid kutwaa ubingwa wa LaLiga kwa mara ya 36 katika historia ya klabu hiyo huku ikiwa na mechi nne mkononi. Hii inamfanya Kiungo wa England, Jude Bellingham, ambaye hadi sasa ana mabao 18 kwenye mechi 26 za LaLiga, kuungana na Waingereza wenzake Laurie Cunningham (msimu wa 1979–80), Steve McManaman (2000–01 na 2002–03), David Beckham (2006-07) na Kieran Trippier (2020-21) ambao wamewahi kutwaa ubingwa wa La Liga.



# Bil.7.2/- kukarabati barabara zilizoathiriwa na mvua

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS), umepokea Sh. bilioni 7.2 za dharura kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara iliyoharibiwa na mvua.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Dodoma, Zuhura Amani, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya wakala huo ndani ya uongozi wa miaka mitatu wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alibainisha kuwa miongoni mwa barabara zitakazokarabatiwa ni ya Dodoma hadi Morogoro katika eneo la Kibaigwa ili kuruhusu magari kupita wakati wote.

"Barabara hii mwaka huu ilijaa maji na kusababisha msongamano wa magari na usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa barabara, tutatumia vizuri fedha hizi ili kuhakikisha turudishe mawasiliano ya madaraja yaliyovunjika wakati wa mvua hizi zilizonyesha juu ya wastani," alisema.

Alisema katika kipindi cha kuanzia Machi 2021 hadi Aprili 2024 wakala huo umeimarisha maeneo mengi yaliyokuwa na hali mbaya ambapo barabara za lami asilimia 81.52 zipo kwenye hali nzuri na asilimia 2.92 zipo kwenye hali mbaya.

Alieleza kwa barabara za changarawe asilimia 56.13 zipo kwenye hali nzuri, asilimia 37.01 zipo wastani na asilimi 6.86 zipo kwenye hali mbaya.

Kadhalika alisema wanatarajia kuanza kujenga barabara za mzunguko wa ndani kilomita 16 li kupunguza msongamano wa magari katikati ya Jiji.

Alisema kazi za usanifu wa kina zinaendelea itakapokamilika ujenzi huo utaanza mara moja ili kupunguza msongamano jijini Dodoma.

Aliongeza kuwa wanatarajia kuanza ujenzi wa Barabara ya Kibakwe Chipogoro (kilomita 75.48) wilayani Mpwapwa itakayojengwa kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha za ndani.

Hata hivyo, alitaja barabara zingine zinazotarajiwa kujengwa mwaka huu kwa kiwango cha lami ni barabara ya Ihumwa hadi Hombolo pamoja na ujenzi wa Daraja la Chilonwa Nzali.




Baadhi ya kinamama wanaouza mboga na matunda jijini Dodoma wakifurahia kongamano lao juzi lililoandaliwa na Mbunge wa Viti Maalumu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Sophia Mwakagenda. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**.

# NEMC yatoa elimu kinga ya afya, uhifadhi wa mazingira

**Na Augusta Njoji**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Kanda ya Magharibi limeanza kukagua na kutoa elimu kwa wafanyabiashara wa chuma chakavu na wachimbaji madini, ili kujiepusha kufanya shughuli zinazohatarisha afya na uhifadhi wa mazingira.

Akizungumza mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha utoaji elimu hiyo kilichofanyika Wilaya ya Igunga, Meneja wa Kanda hiyo inayojumuisha mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi, Edgar Mgila, alisema hatua hiyo inalenga kuwahimiza kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mazingira na Kanuni ya Usimamizi wa Mazingira ya Taka Hatarishi na Taka za Kielektroniki ya mwaka 2021.

Alisema wafanyabiashara wa chuma chakavu wanahifadhi kwenye maeneo ambayo siyo salama, hayajasakafiwa wala kuezekwa.

"Kwa mfano eneo halina sakafu na wala halijafunikwa juu ni rahisi wakati wa mvua kutiririsha sumu ya chuma inayoweza kusababisha madhara kwenye jamii," alisema.

Hivyo, aliwataka kutumia vifaa kinga kwenye ukusanyaji wa taka hizo ili kuepuka kupata magonjwa yanayotokana na sumu hiyo. Kadhalika alisema kwenye ukaguzi migodini wamebaini watu wanaochimba na kuchenjua dhahabu kwa kutumia kemikali hawavai vifaa kinga kuzuia kupata magonjwa mbalimbali ikiwamo saratani.

"Jukumu letu ni kufanya ukaguzi na kutoa elimu kwa wadau na kutoa maelekezo tunapofanya kaguzi, kwa kipindi cha Mei tumefanya ukaguzi Wilaya ya Igunga na Nzega na kutoa elimu ya usimamizi wa mazingira," alisema.

Alifafanua kuwa kwenye utoaji elimu huo wadau wameelezwa umuhimu wa kutumia vifaa kinga na kutumia vizuri kemikali ili zisisababishe madhara kwa binadamu na mazingira.

Alisisitiza kuwa zoezi hilo linaendelea kwenye maeneo mengine ya kanda hiyo ili wafanyabiashara wa vyuma chakavu na wachimbaji ili shughuli za kibinadamu zisiathiri mazingira.

Naye Diwani wa Kata ya Nguvumoja, Alferd Nkuba, alipongeza NEMC kwa kutoa elimu hiyo kwa wachimbaji kuhusu sheria ya mazingira na kanuni zake ili wazingatie usalama wa afya zao na uhifadhi wa mazingira.

Nao viongozi wa wafanyabiashara ya chuma chakavu, Boaz Dhahabu na Idaso Mayanda walipendekeza vibali vya chuma chakavu vitolewe kwa wafanyabishara kulingana na mitaji yao ili kukidhi matakwa ya kanuni.

## Serikali kukuza usawa, kuwawezesha wanawake kiuongozi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema imedhamiria kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake katika uongozi ili kuwa na fursa sawa za uongozi kwenye ngazi za uamuzi.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Hamis, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam kwenye uzinduzi wa mpango 'Think Equal Lead Smart' (TELS) ulioandaliwa na Kampuni ya CEO Roundtable of Tanzania (CEOrt), unaolenga kukuza ushiriki wanawake kwenye fursa za uongozi.

Mwanaidi alisema wanawake wana mchango mkubwa katika maendeleo ya familia na Taifa lakini bado wanakabiliwa na vikwazo vinavyowaathiri na kuwakwamisha katika maendeleo yao ikiwamo mila na desturi.

"Kwa namna ya pekee naupongeza uongozi wa taasisi hii kwa kuendelea kutambua umuhimu wa wanawake na vijana kushiriki katika nafasi za uongozi na maamuzi, nyie ni taasisi ya mfano wa kuigwa kwa maendeleo ya wanawake, na sisi serikali tunaunga mkono juhudi hizi za kumkwamua mwanamke," alisema.

Alisema kinachofanywa na taasisi hiyo kwa kushirikiana na washirika wao ni kuunga mkono dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kutoa nafasi zaidi ya uongozi kwa wanawake.

"Hivi sasa, takwimu zinaonesha kuna ongezeko la mawaziri wanawake kutoka asilimia 15 kwa mwaka 2005 hadi asilimia 37 kwa mwaka 2023, aidha, wabunge wanawake wameongezeka kutoka asilimia 22 hadi kufikia asilimia 37 kwa mwaka 2023."

"Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar wapo asilimia 38, madiwani asilimia 29.9, mabalozi asilimia 25, makatibu wakuu asilimia 22, naibu makatibu wakuu asilimia 28, wakuu wa mikoa asilimia 31, makatibu tawala asilimia 26, wakuu wa wilaya asilimia 33 na wakurugenzi asilimia 28, kwa ujumla haya ni mafanikio makubwa sana kwa wanawake katika kushika nafasi za uongozi na za maamuzi hapa nchini," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa CEOrt, Santina Benson, alisema mpango huo unalenga kuongeza idadi ya viongozi wanawake ngazi ya maamuzi kwenye sekta ya umma na binafsi.

Mwenyekiti wa Vodacom Foundation, Harriet Lwakatare alisema Vodacom wataendelea kufadhili ili kufikia malengo ya mradi huo.



# TANAPA yasimika 'mizizi' ya utalii mikoa Kanda ya Kusini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA), limeanza kuimarisha sekta ya utalii na uhifadhi wa maliasili katika mikoa ya Kanda ya Kusini mwa Tanzania, kwa kujenga ofisi ili kuongeza usimamizi na kuvutia zaidi watalii.

Ofisi hizo zimejengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya na ndiyo ofisi ya kwanza ya kanda za TANAPA kukamilika na kuanza kufanya kazi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ofisi hizo, Kamanda Uhifadhi Kanda ya Kusini, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Steria Ndaga alisema ujenzi wa jengo hilo umegharimu zaidi ya Sh. milioni 891 mpaka kukamilika kwake.

Alisema jengo hilo lina vyumba vya ofisi 19 ambavyo vinatosheleza mahitaji kwa maelezo kuwa kabla ya kujenga jengo hilo walikuwa wamepanga kwenye jengo lenye vyumba vitatu ambavyo vilikuwa havitoshelezi mahitaji.

Kamanda Asteria alisema jengo hilo lilianza kujengwa mwaka 2022 na kukamilika Aprili mwaka huu na kwamba walikuwa wanatumia mfumo wa kutumia mafundi wa mtaani kwa kusimamiwa na wahandisi wa shirika wa kanda na makao makuu.

Alisema eneo walipojenga ofisi hizo walipatiwa bure na Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali na kwamba lina ukubwa wa ekari sita ambazo zote wanakusudia kuzungushia wigo ili kulinda mipaka yake.

"Jengo hili tumelijenga kwa fedha zetu wenyewe ambazo zilikuwa zinaidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shirika na hakuna mfadhili aliyetusaidia na tunaamini kwamba kukamilika kwa jengo hili kutatusaidia kuimarisha shughuli za uhifadhi katika kanda yetu," alisema Kamanda Asteria.

Vilevile alisema ujenzi wa jengo hilo ni utekelezaji wa maagizo ya Bodi ya Wadhamini ya TANAPA ambayo iliagiza kila kanda kujenga ofisi zake na kuanza kuzitumia.

Mkuu wa Wilaya ya Makete mkoani Njombe, Juma Sweda ambaye alimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, alilipongeza shirika hilo kwa kuendelea kuimarisha uhifadhi katika maeneo mbalimbali ya nchi akidai kuwa rasilimali zinazohifadhiwa ni kwa ajili vya kizazi cha sasa na vijavyo.

Alishauri watendaji wa shirika hilo kuendelea kuwashirikisha wananchi kwenye masuala ya uhifadhi ili na wao washiriki kuhifadhi rasilimali hizo kwenye maeneo yao hasa kwa kuhakikisha wanatunza vyanzo vya maji na ikolojia zingine.


Alisema wananchi wa Wilaya za Makete, Mbarali na Chunya wanashiriki vizuri kutunza vyanzo vya maji ambavyo ndivyo vinapopa uhai Mto Ruaha ambao unatumika kwenye shughuli mbalimbali ikiwamo kilimo na uzalishaji wa umeme kwenye mabwawa ya Mtera na Mwalimu Nyerere.

Akizindua ofisi hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Udhamini ya TANAPA, Jenerali Mstaafu George Waitara, aliupongeza uongozi wa shirika hilo Kanda ya Kusini kwa kukamilisha ujenzi wa jengo hilo kwa maelezo ndiyo kanda ya kwanza kukamilisha jengo lake.

Aliagiza kanda zingine tatu zilizobaki kukamilisha haraka majengo yao na kwamba kwa zile ambazo bado hazijaanza ujenzi zikajifunze katika kanda hiyo ya kusini ikiwa ni pamoja na kuitumia ramani ya jengo hilo kama mfano.

Hivyo, aliwataka watendaji wa kanda hiyo kuitumia ofisi hiyo kutoa elimu kwa wananchi kuchangamkia fursa mbalimbali za uhifadhi ikiwemo ujenzi wa hoteli, biashara ya chakula, kuwakarimu wageni pamoja na ajira zinazojitokeza.

Aliwataka wananchi kuchangamkia utalii wa ndani kwa kutembelea vivutio vilivyoko jirani na maeneo yao ili wajifunze na kufurahia maliasili zilizomo.




Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa (wa pili kulia), akiangalia mfano wa hundi ya Sh. bilioni 5.60 iliyotolewa na Benki ya Maendeleo TIB kama mkopo kwa ajili ya uboreshaji mifumo ya huduma za majisafi katika Jiji la Mbeya. Pichani ni Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mbeya UWSA, Cynthia Hilda Ngoye (kulia), Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Lilian Mbassy (wa pili kushoto) na Mkurugenzi wa Miradi wa TIB, Zuwena Hemed (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu wanafunzi kufeli masomo ya sayansi, hisabati yatajwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UKOSEFU wa lishe bora kwa watoto imetajwa kuwa moja ya sababu za kuzorota kwa ufaulu wa masomo ya sayansi na hisabati kwa wanafunzi nchini.

Ofisa Lishe wa Jiji la Mbeya, Itika Mlagalila aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye kongamano la kuimarisha ufaulu na ustawi wa wanafunzi shuleni kupitia lishe toshelevu lililoandaliwa kwa ushirikiano kati ya jiji hilo na Shirika la HELVETAS.

Alisema watoto hao wanakuwa na uelewa mdogo darasani wanapofundishwa na kwamba wakati mwingine huwa wanaichukia shule na kuanza utoro hali ambayo inamfanya kuendelea kuzorota zaidi kielimu.

"Utafiti unaonyesha watoto hawa huwa wanayachukia zaidi masomo ya sayansi hasa hesabu, sasa kipindi kama hiki ambacho tupo kwenye ulimwengu wa sayansi mtoto akianza kuchukia masomo hayo ataishije?" alihoji Itika.

Vilevile alisema tatizo hilo la uelewa mdogo kwa watoto wenye ukosefu wa lishe bora huwa linasababisha watoto hao wakiwa wakubwa kushindwa kuhimili ushindani wa ajira za kimataifa kutokana na uelewa wao kuwa mdogo.

Hivyo, aliwataka wazazi na walezi pamoja na wadau mbalimbali kuhakikisha wanafuatilia lishe za watoto kwa kuhakikisha wanapata lishe bora ili kuimarisha afya zao na uwezo wa kuelewa shuleni.

Mganga Mkuu wa Jiji la Mbeya, Dk. Yesaya Mwasubila, alisema wamebaini kuwa utaratibu wa wanafunzi kula chakula cha mchana shuleni una kasoro mbalimbali kutokana na aina ya chakula ambacho kinaandaliwa kwenye shule hizo.

Alisema shule nyingi watoto wanakula kande na kwamba walipowahoji walimu walisema kuwa chakula hicho ndicho kinapatikana kirahisi na kwa bei nafuu hali ambayo alisema siyo sahihi na badala yake wanatakiwa kuwaandalia watoto chakula bora.

Alisema chakula ambacho watoto wanastahili kukipata ni chenye mchanganyiko wa makundi sita ambayo ni wanga, mafuta, sukari, matunda, mboga na vyakula vya asili ya wanyama.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ili kuhakikisha kila mmoja kwa nafasi yake anashiriki kuimarisha lishe ya watoto shuleni tofauti na ilivyo sasa.

Ofisa Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula Jiji la Mbeya kutoka HELVETAS, Judith Sarapion alisema mradi huo ni matokeo ya ushirikiano wa Jiji la Mbeya na Jiji la Zurich la nchini Uswis na kwamba unatekelezwa kwa miaka mitatu.

Alisema kwa sasa wameshazifikia kata 36 za Jiji la Mbeya ambapo wanahamasisha upatikanaji wa lishe bora kwa wanafunzi wa shule za sekondari na msingi kwa kuwahamasisha wazazi kuchangia chakula na kuhamasisha upandaji wa bustani shuleni.

Meya wa Jiji la Mbeya, Sheikh DorMohamed Issa, alisema Jiji hilo limetunga sheria ndogo ya kuwashurutisha wazazi na walezi kuchangia chakula shuleni baada ya kubaini mwitikio wa uchangiaji huo kuwa mdogo.

# Wakulima Chunya wapewa onyo utoroshaji tumbaku

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAKULIMA wa tumbaku wilayani Chunya mkoani Mbeya, wametahadharishwa kuacha tabia ya kutorosha zao hilo na kwenda kuuza katika maeneo mengine, yeyote atakayekamatwa atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Mrakibu Mwandamizi wa Uhamiaji, Mbarak Batenga alitoa tahadhari hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa anazindua masoko ya tumbaku katika Kata ya Lupa Tingatinga ambapo alisema tumbaku yote inatakiwa kuuzwa kwenye mfumo rasmi.

Alisema mfumo unaotambulika kisheria ni mfumo wa kutumia vyama vya msingi vya ushirika na kwamba kila mkulima anatakiwa kuuza kupitia chama chake ili wakati wa malipo akatwe fedha zote anazodaiwa.

Alisema wakulima watakaokamatwa wakitorosha zao hilo watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria na kwamba wametoa elimu kwa muda mrefu kuhusu kutotorosha zao hilo.

"Kulima umelima wewe, umehudumia mwenyewe lakini ukitorosha tumbaku tutakukamata na kukuchukulia hatua kali sana za kisheria, tumeweka utaratibu mzuri wa kuuza zao hili kwa njia ya ushirika sasa wewe unapotorosha maana yake unahujumu mfumo," alisema Batenga.

Hivyo, aliwataka wakulima hao kila mmoja kuwa mlinzi wa mwenzake kwa kuhakikisha anatoa taarifa kwa viongozi pale anapobaini utoroshaji wa zao hilo ukifanyika.



# Watendaji wavivu wamchefua Katibu Mkuu Kiongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Kiongozi Zanzibar, Zena Ahmed Said, amesema licha ya serikali kuwajali na kuwathamini watumishi wa umma lakini kuna baadhi ya watendaji siyo wawajibikaji.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na watumishi wa umma wa Mkoa wa Kusini Unguja katika hafla ya uzinduzi wa programu iitwayo 'Amshaamsha timiza wajibu' iliyofanyika Tunguu.

Alisema serikali haifurahishwi na baadhi ya watendaji hao na hurudisha nyuma maendeleo ya nchi.

Zena alisema utaratibu wa utumishi wa umma mfanyakazi anatakiwa kuwafanya kazi kwa saa manane ya kazi, lakini wengi wao hawafikishi saa hizo.

Alisema watumishi wengi wa umma wanapofika ofisini hujadili mambo yao binafsi na siyo kuzungumzia utumishi uliyotukuka katika kuwahudumia wananchi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, alisema ndani ya mkoa wake kuna baadhi watumishi wa umma wanakiuka maadili ya kazi hasa ya utoro kwa kuchelewa kuingia ofisini, kauli mbovu kwa wanajamii wanaotaka huduma katika taasisi mbalimbali za mkoa huo.

Alisema watumishi wengi wa mkoa huo hutumia muda mwingi kuzungumza na simu kwa mawasiliano yao binafsi ambayo hayahusiani na masuala ya utumishi, hivyo wakati umefika kwa watendaji hao kubadilika au kufanya maamuzi ya kuacha kazi kwa mujibu wa sheria.

Hivyo alisema atahakikisha anatoa mlo wa asubuhi kwa taasisi zote za serikali katika mkoa huo, ili watumishi kuacha kisingizio cha kutoka mara kwa mara kwenda kutafuta chakula, huku wananchi wakiwa wanasubiri huduma.

Wakichangia katika mkutano huo baadhi ya watendaji wa mkoa huo walisema wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo uhaba wa vitendea kazi, usafiri unaosababisha kuchelewa kufika kazini kwa wakati na malimbikizo ya madeni ikiwamo ya likizo.

# Hifadhi ya Buruge yaleta neema Shule ya Sangaiwe

**Na Rahma Suleiman, aliyekuwa** MANYARA

SHULE ya Msingi ya Sangaiwe iliyopo Wilaya ya Babati mkoani Manyara ni miongoni mwa shule zinazonufaika na uwepo wa ushoroba wa wakuchinja katika Hifadhi ya Wanyamapori ya Burunge, kwa kupatiwa magunia 30 ya mahindi kila mwaka.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Joseph Osole, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) waliofika katika ushoroba huo.

Ziara hiyo ni mwendelezo wa mafunzo ya uhifadhi kupitia mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, ambapo alisema mahindi hayo husaidia watoto kupata chakula shuleni na kusoma vizuri.

Alisema shule hiyo ni miongoni mwa shule mbili zilizomo katika Kijiji cha Sangaiwe na inanufaika kupitia miradi mbalimbali iliyopo kijijini hapo zitokanazo na Hifadhi ya Wanyamapori Burunge.

Alisema kijiji hicho hutoa mahindi kila mwaka kutokana na faida za uwepo wa hifadhi hiyo na wazazi kwa sasa hawachangii chakula.

"Kijiji pia kimeazisha shule nyingine mbili na baada ya miaka mitano mbele baadaye kitakua na shule kama nne ambazo zinasaidia huduma kwa wanajamii kutotembea umbali mrefu kutafuta huduma ya elimu," alisema.

Aidha, alisema licha ya shule hiyo kupatiwa mahindi lakini pia uwepo wa Hifadhi ya Wanyama Burunge pia imepata maendeleo makubwa ikiwamo kupata vifaa kama madawati na mahitaji mengine muhimu, ili kusogeza mbele gurudumu la elimu na kupata maendeleo.

Alisema shule hiyo inawahudumia wanafunzi 714 na mwaka huu wanafunzi wa shule hiyo watafanya mitihani yao ya taifa ya darasa la nne.

Msaidizi wa Mwenyekiti wa Kijiji cha Sangaire, Lucia Gichi, alisema kijiji hicho ni miongoni mwa vijiji 10 vilivyomo katika Hifadhi ya Burunge na kina vitongoji vinne na kaya 976 zenye wakazi 4,091 wakiwemo wanawake 1961 na wanaume 2130.

Alisema ushiriki wa wananchi wa vijiji hivyo katika uhifadhi wa hifadhi ya wanyamapori ni mzuri kutokana na maendeleo wanayopata ikiwamo ujenzi wa shule, zahanati, ofisi ya kijiji, kijiji kulipa posho kwa walimu wanaojitolea katika shule zilizomo katika kijiji hicho na kuwaendeleza watoto 10 wa kijiji hicho elimu ya juu.

Alisema wananchi hao hupatiwa elimu ya uhifadhi na ulinzi wa wanyamapori na kuridhia kukabiliana na ujangili wa wanyamapori katika hifadhi hiyo.

Akizungumzia kuhusu wanafunzi kupatiwa chakula kwa ajili ya mlo wa mchana shuleni hapo, alisema awali wazazi walitakiwa kuchangia chakula, lakini hushindwa kutokana na changamoto za wanyamapori kuharibu mazao yao na upatikanaji wa chakula ulikuwa mdogo na kuamua kuchangia kutokana na kipato kitokanacho na uhifadhi.

Katibu wa hifadhi hiyo, Benson Mwidise alisema hifadhi hiyo hutoa magunia 300 ya mahindi kwa ajili ya shule za msingi zilizomo katika vijiji katika hifadhi hiyo ili wanafunzi wapate mlo wa uhakika wakati wakiwa shuleni wakiendelea na masomo yao.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima (katikati), akizindua NMB Kikundi Akaunti iliyoboreshwa kidigitali. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna na kulia ni Ofisa Mkuu Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali: Tunaendelea kuboresha sheria zinazosimamia habari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inaendelea kuimarisha usimamizi wa sekta ya habari kwa kufanya marekebisho ya sheria, sera na kanuni za kusimamia habari ili kuweka mazingira bora ya wanahabari.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Fatma Khamis Rajab, aliyasema hayo juzi kwamba miongoni mwa juhudi za serikali ni kuweka sera na sheria zitakazohakikisha kutoa uhuru kwa waandishi wa habari bila ya kuathiri uhuru wa mwingine.

Alisema mabadiliko ya sera na sheria za habari yanafanywa hatua kwa hatua ili kuhakikisha inakwenda kwa wakati na kutoa fursa ya upatikanaji wa uhuru wa habari. Hata hivyo, aliwataka waandishi wa habari kutekeleza majukumu yao na kuzingatia misingi ya sheria na kanuni zilizopo hasa kwa jamii kwa mujibu wa mazingira wanayoishi.

Katibu wa Tume ya Utangazaji, Suleiman Abdullah alisema licha ya mchakato mrefu wa Sheria ya Usajili wa Magazeti, Wakala wa Habari Vitabu ya mwaka 1988 na marekebisho yake ya mwaka 1997, tayari imewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu na itawasilishwa katika Baraza la Wawakilishi lijalo kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya kwanza.

Akizungumzia Sheria Namba Saba ya Mwaka 1997 ya Tume ya Utangazaji Zanzibar, alisema wameanza mchakato na tayari wamekutana na wadau kutoa maoni na tayari mchakato huo umewasilishwa katika kamati ya utekelezaji na hatua nyingine zitafuata. Mwanasheria kutoka Tume ya Utangazaji Zanzibar, Khadija Mabrouk alisema ni dhahiri kuwa jitihada za kuimarishwa sekta ya habari zinahitajika kuwekewa miongozo maalumu wa sera, sheria na kanuni zitakazotoa mwelekeo wa utekelezaji wa sekta hiyo.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa habari, serikali imepunguza gharama za usajili na kupata leseni pamoja na ada ya malipo. Mratibu wa Baraza la Habari Tanzania upande wa Zanzibar Shifaa Said, alisema muda mrefu umepita na hakuna matumaini yoyote ya mabadiliko ya sheria zilizopo ambazo zinakwaza uhuru wa habari na kuathiri tasnia hiyo, hivyo alishauri ni vyema kufanyiwa marekebisho kwa maslahi ya umma.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**LUQMAN ISSA MWANYERO** anatangaza kupotelewa kwa hati ya kusafiria yenye namba TAE 382807 iliyotolewa uhamiaji makao makuu uhamiaji. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/76919/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RAMADHANI NASSORO RAMADHANI a**natangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC 981 DSL.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DOD/DOD/16062/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CRISPIN .B. KAMUNTU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA CROWN yenye namba T 606 ECK, CHASSIS NAMBA: GRS2000011414 na ENGINE NAMBA: 4GR0485726. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIG/76683/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MICHAEL GODSON NGOYE** anatangaza kupotelewa na kadi zake za pikipiki zenye namba za usajili: MC 437 BDA aina ya KING LION yenye Engine Na.KL162FMIIII46922. MC 458 BDA SAUND yenye Engine Na. 162FMJB5057525. T.470 BJE SAUND yenye Engine Na. 156FM12A5066435. Kwa yeyote atakayeziona anaombwa kutoa taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu.

Taarifa Polisi: **PAN/B.1/19/VOL.11/01.**

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF BABATI**
**AT BABATI**
**CIVIL CASE NO. 01 OF 2024**
**BANK OF AFRICA TANZANIA LIMITED ............PLAINTIFF**
**VERSUS**
**NESTORY TILLYA PATRICK......DEFEDANT**
**NOTICE OF HEARING/ MENTION**
**TO NESTORY TILLYA PATRICK**
**C/O:............**

TAKE NOTICE that the above CIVIL CASE has fixed for Mention in District Court of BABATI on 14th day of May, 2024 at 08:30 a.m. O'clock in the forenoon.
You may appear in person or by advocates of agent duly authorized to me and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to ready in support your cases.
TAKE FURTHER NOTICE THAT in default of your appearance on that day before mention or hearing, the case will proceed in your absence.
Given under my hand and the seal of the court this 2nd day of May, 2024

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
BABATI DISTRICT COURT

**IN THE DISTRICT COURT OF MONDULI**
**AT MONDULI**
**CIVIL CASE NO 01 OF 2024**
**BETWEEN**
**BANK OF AFRICA TANZANIA LTD.........APPELANT**
**VERSUS**
**CALVIN PETER MUSHI ............DEFENDANT**

**NOTICE OF MENTION**
**TO: CALVIN PETER MUSHI**

TAKE NOTICE That the above case has been fixed for mention in the court at Monduli on the 04 day of JUNE 2024 at 8:30 a.m in the forenoon.
You may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all documents upon which you intended to rely in support of your case.
TAKE FURTHER NOTICE THAT in default of your appearance on that day and time before mention or hearing the court may proceed in your absence.
A copy of the bill of costs/chamber summons/affidavit/petition od appeal/judgement and decree is attached to
GIVEN under my HAND and SEAL of the court this 03 day MAY 2024

HAKIMU MKAZI WA WILAYA MONDULI
RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF KINONDONI**
**AT KINONDONI**
**COMMERCIAL CASE NO 5107 OF 2024**
**BANK OF AFRICA............PLAINTIFF**
**VERSUS**
**OSCAR MBEKENGA LUFURANO...............DEFENDANT**
**TO: OSCAR MBEKENGA LUFURANO**
**NOTICE DATE FOR MENTION**

THE NOTICE that the above case has been fixed for mention on 07 day Of MAY 2024 at 08:30 a.m.
Before Hon. VENERANDA KASEKO
YOU ARE required to appear in this court without failing and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
Given under my Hand and the Seal of the Court this 02 day of MAY 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF KINONDONI**
**AT KINONDONI**
**COMMERCIAL CASE NO 5106 OF 2024**
**BANK OF AFRICA..........APPELANT**
**VERSUS**
**WITNESS ROBINSON SHOO.........RESPONDENT**
**TO: WITNESS ROBINSON SHOO**
**NOTICE DATE FOR MENTION**

THE NOTICE that the above case has been fixed for mention on 07 day Of MAY 2024 at 08:30 a.m.
Before Hon. VENERANDA KASEKO
YOU ARE required to appear in this court without failing and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
Given under my Hand and the Seal of the Court this 02 day of MAY 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 6073/2024**
**In the matter of the Estate of the late**
**ALOYCE MATEI MALULA**
**of Vikonje B within Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY VERONICA JOSEPH DEDE**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 10TH Day of MAY, 2024
Presented for filling this 08th Day of APRIL, 2024.

PRINCIPAL / SENIOR RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT COURT
RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 7657/2024**
**In the matter of the Estate of the late GIFT STANFORD MAKALA of Ihumwa within Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**SARAH AMOS NJOGHOMI**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 PROBATE RULES GN. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 07 Day of 05, 2024
Date at Dodoma this 19 Day of 04, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 7344 OF 2024**
**In the matter of the Estate of the late**
**MWANAKOMBO MAHARAGE CHANDE**
**And**
**In the Matter of Application for letters of Administration by RAJAB WILLIAM MWAKIMI**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 27 day of 05, 2024
Dated at DAR ES SALAAM this 01 day of 05, 2024

Senior Resident Magistrate

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...22/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: HASSINA ABDALLAH wa MLAPAKOLO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA NAUSHAD ISMAIL IBRAHIM**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 14 Mwezi 05 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 2 mwezi 05 mwaka 2024

HAKIMU

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 9199 OF 2024**
**In the matter of the Estate of the Late**
**RAMAN DEEP BHATIA**
**And**
**In the Matter of Application for letters of administration by MANPREET KAUR BHATIA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner
Objections to the grant should be filed on or before the 4th day of June 2024
Dated at DAR ES SALAAM this 29th day of April 2024

Senior Resident Magistrate

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Waliofariki mafuriko Brazil wafikia 56

**PORTO ALEGRE, Brazil**

SHIRIKA la Ulinzi wa raia la Brazil limesema idadi ya vifo kutokana na mafuriko na maporomoko ya udongo yaliyosababishwa na dhoruba kali kusini mwa Brazili imepanda hadi kufikia watu 56.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na shirika hilo, kuongezeka kwa viwango vya maji katika jimbo la Rio Grande do Sul kulikuwa kukiyafurisha mabwawa na kutishia jiji kuu la Porto Alegre.

Ilielezwa kuwa wakati viongozi wa mji huo wakihangaika kuwahamisha watu kwenye baadhi ya vitongoji vilivyokuwa vimezama, makazi mengi yalionekana kuharibiwa vibaya.

Zaidi ya watu 24,000 walilazimika kuyahama makazi yao kutokana na hali hiyo ya mafuriko. Huku mamlaka zikisema mvua kali na mafuriko yameathiri zaidi ya manispaa 265 huko Brazil.

*DW*



Wakazi nchini Kenya wanaoishi kando ya mto wakiokota baadhi ya mabaki ya mali zao baada ya makazi yao kubomolewa kwa amri ya serikali jana. **PICHA: MTANDAO**

# Serikali Kenya yaagiza nyumba kubomolewa

**NAIROBI, Kenya**

KATIKA Kaunti ya Nairobi nchini Kenya mamia ya watu wameshuhudia nyumba zao zikibomolewa ikiwa ni utekelezaji wa agizo la serikali kwa mtu yeyote anayeishi karibu na mito kuacha makazi yake na kuhamia maeneo ya juu baada ya mvua kubwa na mafuriko, ambayo yamesababisha athari kubwa katika eneo hilo.

Serikali nchini humo ilisema ubomoaji huo ulikuwa muhimu ili kuzuia vifo zaidi, kutokana na kuwa vitongoji vingi vilijengwa kando ya mito, ikisema kuishi ndani ya mita 40 kutoka kwenye kingo za mto ni kinyume cha sheria.

Hapo awali, mamlaka iliwapa watu katika maeneo yaliyotengwa saa 24 kuhama, na kwamba tarehe ya mwisho ilikuwa ni Mei 3, mwaka huu, huku wakazi wengi wakiiambia BBC kwamba walipatwa na mshangao kwamba nyumba zao zilibomolewa kabla ya muda uliowekwa.

Nicholas, ambaye ni mfanyakazi wa kawaida, alieleza kuwa alifika nyumbani kutoka kazini na kukuta nyumba yake ikiwa imeharibika „Inauma sana. Walipaswa kutupa muda wa kupata pesa na kufikiria jinsi ya kujipanga angalau. Lakini kutupa taarifa fupi, na tunafanya kazi, sio haki hata kidogo“.

Mama wa watoto wawili Phylis alisema alikuwa akijaribu kujua mahali pa kwenda na jinsi ya kusafirisha mali ambayo alifanikiwa kuokoa.

„Nina watoto, hawajala chochote. Mimi ni mama ninayelea watoto peke yangu... wameharibu maisha yetu,“ alisema kwa hasira.

Walioshuhudia ubomoaji huo waliiambia BBC kuwa jeshi lilihusika, huku picha zilizochapishwa na vyombo vya habari zikionekana kuonesha wanaume wakiwa wamevalia mavazi ya kijeshi wakisimamia uvunjaji huo.

Msemaji wa serikali Isaac Mwaura alisema „Hawa ni watu walewale wanaokufa. Hawa ni watu ambao wanaathirika na mafuriko haya. Wakati mwingine maji yanapopungua basi watu wanarudi kwenye majengo yao. Kwa hiyo kama serikali inabidi tuwe wazi sana na dhahiri“.

Licha ya maeneo hayo ya kitongoji cha Mukuru Wa Reuben kuonekana kuharibiwa na mafuriko, huku serikali ikiendelea kutoa hadhari, wakazi kama Nicholas walisema wataweka kambi karibu na nyumba zao zilizoharibiwa kwa kuwa hawana mahali pengine pa kwenda.

Serikali inasema imewahamisha watu chini ya 27,600 waliolazimishwa kutoka kwenye makazi yao na mafuriko katika kambi mpya zilizojengwa.

Takribani watu 210 kote nchini humo wamefariki kutokana na mafuriko hayo, huku wengine 90 wakiwa hawajulikani walipo, kulingana na makadirio rasmi ya hivi karibuni.

Ilieleza kuwa wiki moja iliyopita zaidi ya watu 50 walipoteza maisha wakati wa wimbi la maji lilipopitia vijiji karibu na mji mkuu wa Nairobi, huku mvua kubwa ikitabiriwa kuendelea kwa mwezi mzima, mamlaka zikionya kuwa mabwawa 178 yana hatari kubwa ya kufurika.

Rais William Ruto alionya kuwa huenda taifa hilo likakumbwa na kimbunga cha kwanza kabisa, huku Hidaya kikizidi kushika kasi katika baadhi ya maeneo ya Tanzania. Huku akiamuru shule zifungwe kwa muda usiojulikana.

Huko Nairobi, Phylis, ambaye tayari amelazimika kuondoka nyumbani kwake, alihimiza mamlaka kuwa na mpango thabiti linapokuja suala la kuhama, akisema „Serikali ikitubomolea nyumba angalau itupe suluhu, watuambie tuelekee wapi, hatujui pa kwenda,“ alisema.

*BBC*

## DRC yaendelea kuishutumu Rwanda

**KINSHASA, DRC**

MSEMAJI wa serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) Patrick Muyaya amelishutumu Jeshi la Rwanda na kundi la M23 kwa madai ya kutekeleza shambulizi baya zaidi nchini humo.

Ilielezwa kuwa Rwanda leo pia ilipuuza madai ya Marekani kwamba vikosi vyake vilihusika katika shambulio baya dhidi ya kambi ya wakimbizi mashariki mwa DRC.

Vyanzo vya ndani vilibainishwa kuwa takriban watu kumi waliuawa katika milipuko siku ya Ijumaa kwenye kambi hiyo iliyoko nje kidogo ya mji wa Goma.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ilisema katika taarifa yake kuwa inalaani vikali shambulio hilo kutoka Kikosi cha Ulinzi cha Rwanda (RDF) na kundi la M23 lililofanyika katika kambi ya Mugunga.

Wakati huo huo, msemaji wa serikali ya Rwanda, Yolande Makolo katika ujumbe wake kwenye mtandao wa X, zamani ukijulikana Twitter, aliyataja matamshi hayo ya Marekani kuwa hayana msingi.

*VOA*

## Mashirika yapinga muswada kuhalalisha ukeketaji Gambia

**BANJUL, Gambia**

MASHIRIKA mbalimbali ya kiraia ikiwamo Muungano wa Wanawake wa Kiafrika unaopinga ukatili na unyanyasaji unaohusishwa na mila, umeandaa maandamano kukataa mapendekezo ya mbunge huko Gambia ya kupitisha muswada unaokubali suala la ukeketaji kwa wanawake.

Ilielezwa kuwa nchini Gambia, ambako ukeketaji umepigwa marufuku tangu mwaka 2015, mbunge aliwasilisha muswada mwanzoni mwa Machi mwaka huu ili kufanya kitendo hiko kuwa halali tena.

Pendekezo hilo limekataliwa vikali na vyama vingi, haswa muungano wa mashirika unaopinga ukeketaji.

Akihojiwa na RFI, Mame Konaté, katibu mkuu wa muungano huo anatoa wito wa kukaa mbele ya Bunge la Gambia dhidi ya maamuzi ya uhalifu dhidi ya wasichana.

"Ni hisia ya hofu ambayo inatuingia kwa sababu tunajiambia kwamba, ikiwa tutaanza kupoteza mafanikio ambayo mama zetu walipigania kwa miaka kadhaa, inakuwa hatari sana kwetu," alisema.

"Pia ina maana ya kusema hapana, kupitia hatua zilizochukuliwa, kwa kufutwa kwa sheria dhidi ya ukeketaji nchini Gambia. Inamaanisha pia kuzindua kampeni ya uhamasishaji na kuandaa msafara wa kwenda Gambia na ikiwa ni lazima, kufanya kikao.

*RFI*

HABARI MICHEZO

# MABINGWA BETIKA MBEYA TULIA MARATHON KUJAZWA MAMILIONI

**Mwandishi Wetu**

WAKATI amshaamsha ya mbio ya Betika Mbeya Tulia Marathon leo ikifanyika jijini Dar es Salaam, ikiongozwa na Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma, mshindi wa msimu huu ametengewa kitita cha shilingi milioni tatu, imeelezwa.

Mbio hizo zinazodhaminiwa na Kampuni ya Michezo ya Kubashiri Matokeo ya Betika, zitafanyika Ijumaa na Jumamosi ijayo kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Tayari amshaamsha kuelekea jijini Mbeya kwenye msimu wa saba wa mbio hizo zinaendelea kwenye mikoa mbalimbali ambapo leo zitafanyika jijini Dar es Salaam.

Spika wa Bunge la Jamburi ya Muungano Tanzania, Dk. Tulia Ackson, alisema amshaamsha hizo ikiwamo iliyofanyika jijini Dodoma juzi, ni sehemu ya maandalizi kuelekea kwenye mbio za Betika Mbeya Tulia Marathon msimu huu.

Ofisa Habari wa Taasisi ya Tulia Trust, Joshua Edward, alisema juzi kwamba mshindi wa marathon kwa wanaume na wanawake kila mmoja ametengewa kitita cha shilingi milioni tatu huku washindi wa pili kila mmoja akizawadiwa shilingi milioni mbili na watakaoshika nafasi ya tatu kuondoka na milioni moja moja.

„Kuna zawadi ya pesa taslimu kwa watakaomaliza nafasi ya nne hadi 10 kwenye marathon," alisema Edward na kuongeza kwamba bingwa wa nusu marathon pia ataondoka na kitita cha shilingi milioni mbili kwa kila upande.

„Huku pia tutatoa zawadi kwa watu 10 watakaomaliza mwanzo, wale wa mbio za uwanjani pia watakaomaliza nafasi za juu watazawadiwa pesa taslimu," alisema.

Mbio hizo zinazotarajiwa kushirikisha wanariadha zaidi ya 5,000 zitaongozwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, zikilenga kukusanya fedha kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya afya na elimu mkoani Mbeya na maeneo mengine.

Tofauti na misimu iliyopita, msimu huu hamasa imeongezeka kwa baadhi ya mikoa kufanya mbio za amshaamsha ambapo leo ni Dar es Salaam na watakaofanya vizuri watagharamiwa na Betika kwenda Mbeya kushiriki mbio hizo.

Mjini Iringa amshaamsha ilikuwa jana wakiongozwa na Meya wa Manispaa, Ibrahim Gwada, ambaye aliwakabidhi bendera ya mabingwa na ile ya Tulia Trust washiriki wa mkoa huo watakaokwenda Mbeya kwenye Mbio ya Tulia Marathon.

Ofisa Habari wa Betika, Rugambwa Juvenalius, alisema, wakimbiaji hao watagharamiwa na Betika ili kuongeza hamasa.

„Betika itawagharamia washiriki 460 wa mikoa ya Mbeya, Dar es Salaam, Mtwara, Dodoma, Iringa, Rukwa na Morogoro ambao wanashiriki mbio za hamasa tayari kwa ile ya Betika Tulia Marathon msimu huu," alisema.



Meya wa Iringa, Ibrahim Gwada (mwenye suti ya michezo katikati), akifurahia na baadhi ya wakimbiaji wa Iringa baada ya kushiriki mbio ya amshaamsha ili kujiweka fiti tayari kushiriki kwenye msimu wa saba wa Betika Mbeya Tulia Marathon Mei 10 na 11, mwaka huu jijini Mbeya. Mbio za amshaamsha zilifanyika juzi mjini humo. **MPIGAPICHA WETU**

# Mfungaji bora Championship lulu Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

MFUNGAJI Bora wa Ligi ya Championship, Edger William wa KenGold, ameonekana kuwa lulu kwa klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara na tayari zimeanza kuwania saini yake, imeelezwa.

Edger, ambaye mabao yake 21, yamechangia kwa kiasi kikubwa timu hiyo kupanda Ligi Kuu, amesema ameanza kupokea ofa kutoka kwa klabu mbalimbali ambazo hakuwa tayari kuzitaja, lakini akisema kipaumbele chake kwanza atakiweka kwenye timu yake hiyo yenye maskani yake, Chunya mkoani Mbeya.

„Ni kweli kuna klabu kama tatu hivi za Ligi Kuu zimekuja kwangu zinanitaka, unajua mpira ni kazi kama kazi zingine na haya ni maisha, sijakubali wala kukataa, kwanza kabisa naisikilizia klabu yangu hii ambayo nimeipandisha, kama ikikubali ninachohitaji basi nitasalia, kama haikuwezekana basi nitakwenda kutafuta malisho sehemu nyingine, lakini mimi napenda kusalia hapa kama tukikubaliana," alisema Edger.

Akizungumzia kupanda kwa klabu yake, alisema hali ilikuwa ngumu, ya presha na wakati mwingine kukatisha tamaa.

„Asikwambie mtu, msimu huu ligi ilikuwa ngumu sana, kwa sababu hata nyinyi mkishinda, wenzenu mnaotaka kupanda nao daraja nao wanashinda pia. Halafu ukiangalia pointi zinakaribiana, hii ilikuwa inasababisha wasiwasi, presha kwa wachezaji, mashabiki wa viongozi, mpaka tumepanda, we acha tu, wacha kwanza tupumzike," alisema straika huyo.

Mbali na kupanda daraja, KenGold ndiyo mabingwa wa Championship, baada ya kumaliza ligi hiyo wakiwa kinara kwa pointi 70.

Wakati straika huyo akiwa na mabao 21, anafuatiwa na Boban Ziruntusa wa Biashara United mwenye 20, Oscar Mwajanga wa Mbeya Kwanza (19), Maulidi Shaaban wa Mbeya City (17), Frank Francis wa TMA (15), Haruna Chanongo wa Pamba na Kilaza Mazoea na Cosmopolitan, mabao 12 kila mmoja, Abdulaziz Shahame wa TMA, na Mishamo Daud wa KenGold kila mmoja akicheka na nyavu mara 10.

## Kundemba FC yazidi kutepeta

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

HALI ya Kundemba FC imeendelea kuwa mbaya baada ya kupokea vipigo mfululizo katika Ligi Kuu Zanzibar inayoendelea visiwani hapa.

Katika michezo miwili ya ligi hiyo iliyopita, Kundemba FC imepoteza na kuendelea kujichimbia katika mstari wa kushuka daraja kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar yenye timu 16, hivyo kuwa miongoni mwa timu nne zilizopo katika mstari hatari wa kushuka daraja ambapo ipo nafasi ya 13 ikiwa na alama 20.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mohmed Seif ‚Kocha King', ambaye ameanza kukinoa kikosi hicho katika mchezo wao wa juzi dhidi ya Kipanga FC na kuambulia kichapo cha mabao 2-1, alisema kilichokosekana katika kikosi hicho ni mwamko wa wachezaji. Alisema kwa kuwa timu hiyo imepokea mlolongo wa matokeo mabaya ndio sababu kubwa wachezaji wamekosa hamasa, hivyo kinachohitajika ni kuwatia moyo jambo ambalo analifanyia kazi kwa sasa.

"Timu ipo vizuri na inacheza vizuri, kikubwa wachezaji hawana hamasa na hii pengine inatokana na kutopata matokeo mazuri kwa muda mrefu," alisema.

## Kocha Mafunzo akiri ligi ngumu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Msaidizi wa timu ya Mafunzo SC, Abdalla Bakari ‚Edo', amesema hakuna mchezo rahisi katika michezo hii kumi iliyobaki ya kumalizia msimu wa Ligi Kuu Zanzibar 2023-2024.

Mafunzo SC ni miongoni mwa timu ambazo mipango yao mikubwa ni kuhakikisha inamaliza ligi hiyo ikiwa katika nafasi nne za juu.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema mipango yao haipo katika mbio za ubingwa bali ni kuhakikisha timu hiyo inamaliza nafasi nne za juu mwishoni mwa msimu wa ligi hiyo inayodhaminiwa na PBZ.

Mafunzo SC juzi ilitoka sare ya pili mfululizo baada ya kutoshana nguvu ya bao 1-1 dhidi ya Maafande wenzao wa KVZ FC

Edo alisema kulingana na ugumu wa ligi yenyewe mpaka sasa timu hiyo inajikita zaidi kupata pointi ambazo zitaisogeza katika nafasi nne za juu.

Akizungumzia mchezo wao wa 22 dhidi ya KVZ FC, alisema ulikuwa mgumu kwa kuwa wapinzani wao wapo katika mbio za ubingwa na michezo yote ni muhimu kwao.

## ZISIKUPITE

### TEN HAG KUMRITHI TUCHEL

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, ndiye anayetarajiwa kuchukua nafasi ya Thomas Tuchel anayeondoka Bayern Munich. ***(Falk Christian)***

### NUNEZ ALENGWA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 24, analengwa na Barcelona msimu huu kama mbadala wa mshambuliaji wa Poland, Robert Lewandowski, 35. ***(Sun)***

### ANTONY ASUBIRIWA KUUZWA

MANCHESTER United inasubiri ofa kwa winga wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 24, huku wakitafuta nafasi katika kikosi chao kumnunua kiungo wa kati wa Kimataifa wa Ufaransa na Crystal Palace aliyezaliwa England, Michael Olise mwenye miaka 22. ***(Rudy Galetti).***

### VLAHOVIC AITAKA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Juventus na Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 24, anavutiwa na Arsenal huku Mikel Arteta akijaribu kuimarisha safu yake ya ushambuliaji. ***(Tuttosport)***

### RAYA MKATABA WA KUDUMU

ARSENAL ina makubaliano ya mazungumzo na Brentford kukamilisha usajili wa kudumu wa mlinda mlango wa raia wa Hispania, David Raya mwenye umri wa miaka 28, msimu huu kwa pauni milioni 27. ***(Fabrizio Romano)***

### WATAREJEA SIKU ZIJAZO

LIVERPOOL ina matumaini kuwa Kocha Msaidizi Pep Lijnders, ambaye anatazamiwa kuondoka msimu huu pamoja na Jurgen Klopp, watarejea Anfield siku zijazo. ***(Mirror)***

### MAGUIRE AWEKWA CHAMBO

KLABU ya Manchester United inatarajia kumtumia mlinzi wa England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 31, msimu huu kama chambo cha kuwashawishi Everton kuwauzia mlinzi wao, Jarrad Branthwaite, 21. ***(Star)***

### WILLIAM KUZUIWA KUONDOKA

KOCHA wa Palmeiras, Abel Ferreira, anataka rais wa klabu hiyo, Leila Pereira, kuzuia kuuzwa kwa winga wa Brazil, Estevao Willian, mwenye umri wa miaka 17 kwenda Chelsea, ambao wameweka mezani ofa ya euro milioni 55. ***(Goal)***

### GRAHAM ATAJWA AJAX

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Graham Potter, yuko katika kinyang'anyiro cha kuinoa Ajax baada ya mabingwa hao mara nne wa Ulaya kukata tamaa ya kurejea tena kwa Ten Hag wa Manchester United. ***(De Telegraaf)***

### QUANSAH MKATABA MPYA

MLINZI wa England, Jarell Quansah mwenye umri wa miaka 21, yuko mbioni kupata mkataba mpya wa muda mrefu baada ya kuonesha kiwango kizuri msimu wake akiwa Liverpool. ***(Mirror)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# HAALAND HAZUILIKI EPL

## Guardiola asema pointi tisa watakuwa mabingwa lakini saba ama sita Arsenal...

**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Manchester City, Erling Haaland, alifunga mabao manne huku klabu hiyo ikisalia kwenye mkondo wa kushinda taji la nne mfululizo la Ligi Kuu England wakati ikishinda mabao 5-1 dhidi ya Wolverhampton Wanderers Jumamosi.

Saa chache baada ya ushindi wa mabao 3-0 wa Arsenal dhidi ya Bournemouth, vijana hao wa Pep Guardiola walijibu kwa ushindi huo mnono ambao uliwavuta kwa pointi moja nyuma ya 'Washikabunduki' hao wa London Kaskazini waliopo kileleni mwa msimamo.

Arsenal wana pointi 83 wakati mechi mbili zikisalia katika moja ya mbio kali za ubingwa kwa miaka mingi, huku City wakiwa na 82, lakini wamesalia na mechi tatu.

"Pointi tisa zaidi, tutakuwa mabingwa. Pointi saba, pointi sita, pointi tatu, Arsenal itashinda Ligi Kuu," alisema Guardiola.

"Ikiwa tutashinda michezo, tutakuwa mabingwa, wachezaji wanajua na tunapaswa kufanya hivyo tena na tena na tena."

Haaland mwenye umri wa miaka 23, aliongeza uongozi wake wa kufunga mabao kwenye ligi hadi 25.

Alianza kufunga kwa mkwaju wa penalti dakika ya 12 na la pili dakika ya 35 baada ya kupaa juu na kufunga kwa kichwa akiunganisha krosi ya Rodri.

"Hilo ni goli zuri. Baba yangu (Alf-Inge Haaland, ambaye aliichezea City) atafurahia hilo," alisema Haaland akiiambia Sky Sports.

"Si mbaya, mabao 25 msimu huu. Tunaendelea."

City itacheza mechi mbili za ugenini huko Fulham na Tottenham Hotspur kisha kufunga msimu nyumbani dhidi ya West Ham United.

Arsenal itasafiri hadi Old Trafford kucheza na Manchester United kabla ya kuwakaribisha Everton siku ya mwisho.

# MADRID MABINGWA TENA LALIGA 2023/24

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid imeshinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumamosi kwa kuifunga Cadiz kabla ya wapinzani wao Barcelona kupoteza kwa Girona na kuipa Madrid uongozi usioweza kufikiwa kileleni.

Ushindi mzuri wa Madrid wa mabao 3-0 dhidi ya Cadiz katika Uwanja wa Bernabeu ulimaanisha kuwa wamefikisha pointi 87 katika michezo 34.

Girona waliwafunga Barca mabao 4-2 huko Montilivi na kusonga hadi nafasi ya tatu, pointi 14 zikiwa zimesalia mechi nne pekee.

Miamba hao wa Hispania bado wanaweza kubeba Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, huku wakijiandaa kukabiliana na Bayern Munich katika mchezo wao wa mkondo wa pili wa nusu fainali Jumatano. Timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2 katika mechi ya kwanza.

Akizungumza baada ya kutwaa taji hilo, Kocha wa Madrid, Carlo Ancelotti, alisema timu yake itasherehekea kwa wakati ufaao, lakini alitaka kuangazia nusu fainali kwanza.

„Tuna furaha sana. Mashabiki wetu wote wana furaha sana. Tulistahili taji hili na tungependa kusherehekea na mashabiki wetu,“ alisema Ancelotti.

„Lakini nadhani mashabiki wanaweza kuelewa kwamba tuna changamoto kubwa Jumatano na tunapaswa kujiandaa kwa hilo, ili kuwapa furaha zaidi mashabiki. Tutasherehekea ubingwa wa LaLiga wikendi ijayo.

„Kesho tunafanya mazoezi, kila mtu anaweza kufanya anachotaka. Tunapaswa kuzingatia mchezo wa Jumatano.“

Mashabiki wengi wa Madrid walikusanyika karibu na Bernabeu baada ya matokeo ya Barca kuwasalimia wachezaji walipokuwa wakiondoka uwanjani, akiwamo Jude Bellingham na Rodrygo Goes.

Taji la ligi ya 2023-24 ni la 36 kwa Madrid, na kuendeleza rekodi yao ya kuwa na timu iliyolitwaa mara yingi zaidi kuliko timu yoyote ya LaLiga.




## Xavi abaini mapungufu Barcelona



**BARCELONA, Hispania**

XAVI Hernandez amesema kichapo cha Jumamosi cha mabao 4-2 kutoka kwa Girona kilikuwa ishara ya mapungufu ya Barcelona msimu huu, lakini akasisitiza kuwa timu yake imekuwa bora katika mechi zao nne dhidi ya wapinzani wao hao wa Katalunya na Real Madrid.

Ushindi wa Girona mjini Montilivi uliwapa nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza katika historia ya klabu hiyo ya Katalunya, huku pia ukimaanisha Real Madrid kutawazwa mabingwa wa LaLiga kukiwa na michezo minne iliyosalia.

Barca, wakati huo huo, wameshuka hadi nafasi ya tatu kwenye jedwali, chini ya Girona.

„Nimehuzunika sana na nimesikitishwa kwa sababu tumeona pande zote mbili za sarafu katika mchezo mmoja,“ alisema Xavi katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

„Niliridhika sana wakati wa mapumziko kwa sababu tulikandamiza vema na kuwatawala Girona, jambo ambalo ni gumu sana, labda hadi dakika ya 60. Kutoka hapo, ni muhtasari wa msimu wetu.

„Na kisha ni kuhusu makosa. Tulikuwa na mchezo chini ya udhibiti, lakini kwa mara nyingine tena inakuja kwa makosa.“

Andreas Christensen na Robert Lewandowski walikuwa wameipa Barca uongozi wa mabao 2-1 hadi mapumziko, Girona ikijibu kupitia kwa mfungaji bora wa LaLiga Artem Dovbyk.

Hata hivyo, mchezo uliyumba katika kipindi cha pili kutokana na mabao ya Miguel Gutierrez na bao la pili kutoka kwa mchezaji wa akiba Portu katika dakika 30 za mwisho Girona wakijikatia tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa msimu ujao.

Barca sasa wamepoteza mechi zote mbili za ligi dhidi ya Girona msimu huu kwa mara ya kwanza, wakifungwa mara nane katika mchakato huo, huku pia wakifungwa katika mechi zote mbili za El Clasico dhidi ya Madrid.


Hata hivyo, Xavi alisema anaamini matokeo hayo hayaakisi uwiano wa uchezaji katika mechi hizo.

„Katika mechi nne dhidi ya timu mbili zilizo juu yetu, Madrid na Girona, tumekuwa bora,“ bosi wa Barca alisisitiza.

„Lakini haijaoneeshwa kwenye alama na tumepoteza zote nne, kwa hiyo lazima tuboreshe zaidi.“

Msimu wa Barca utaisha bila taji, lakini bado wanashindania nafasi ya pili na Girona na nafasi ya kucheza Super Cup msimu ujao.

## Greenwood kubaki Getafe




**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imefanya mazungumzo na Getafe juu ya kuongeza mkataba wa mkopo wa Mason Greenwood na timu hiyo ya Hispania, kwa mujibu wa ESPN.

Greenwood alijiunga na Getafe kwa mkataba wa miezi 12 msimu uliopita wa majira ya joto baada ya kuondolewa mashtaka ya ubakaji na unyanyasaji dhidi yake, na amefurahia muda wake nchini Hispania kwa mabao kumi na kusaidia sita katika mechi 32 alizocheza.

Mkataba wake wa mkopo haujumuishi kipengele cha kudumu cha uhamisho, lakini Getafe wamekiri waziwazi nia yao ya kumrejesha mchezaji huyo wa miaka 22 msimu ujao.

Kwa mujibu wa The Athletic, mazungumzo yamefanyika juu ya mkataba mwingine wa mkopo ambao utafanya Greenwood kusalia na Getafe kwa kampeni ya 2024/25.

Kwa hali ilivyo, United wangependelea mauzo ya kudumu, lakini kuna imani kwamba Getafe hawatafuata hatua hiyo.

HABARI MICHEZO

# ABSA YAAHIDI KUENDELEZA DAR CITY MARATHON, ZAFANA

Na Somoe Ng'itu

WAKATI Absa Dar City Marathon 2024, zikitimua vumbi lake jijini Dar es Salaam jana, katika hali ya hewa ya utulivu baada ya tishio la kimbunga Hidaya kupoteza uwezo wake kwa mujibu wa taarifa kutoka mamlaka husika, wadhamini wakuu wa mbio hizo Benki ya Absa Tanzania, wameahidi kuendeleza udhamini wao.

Ikiwa ni mara ya nne kufanyika mbio hizo chini ya udhamini mkuu wa Benki ya Absa Tanzania, mtifuano huo ulishuhudiwa wanariadha zaidi ya 3,000 wakifukuza upepo katika mitaa ya katikati ya Jiji la Dar es Salaam huku lengo lake likiwa ni kusaidia upatikanaji wa vifaatiba kwa ajili ya wodi ya wanawake ya Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na kutangaza vivutio vya utalii vipatikanavyo katikati ya jiji hilo.

Akizungumza baada ya kufanyika mbio hizo, Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Absa Tanzania, Aron Luhanga, alisema kutokana na mafanikio ya mbio hizo, benki hiyo itaendelea kuwapo kwa kipindi kirefu katika kudhamini mbio hizo.

"Kama ahadi ya chapa yetu isemayo ,Tunadhamini Story Yako', Benki ya Absa itaendelea kuthamini stori za maisha ya Watanzania, kwani sehemu ya mapato ya mbio hizi yatakwenda kusaidia jamii kwa kuwezesha upatikanaji wa vifaatiba kwa ajili ya wanawake na watoto.

"Absa tunaamini kuwa mtu yeyote anaweza kuandika stori yake kutokana na mazoezi na kukimbia ni moja ya mazoezi, lakini pia tunaamini utajiri upo kwenye afya, na kukimbia kunaleta afya. Jamii na nchini itapiga hatua kubwa ya kimaendeleo kukiwa na watu wenye afya bora, Absa tupo kuhakikisha stori hizo zinaandikwa kwa ufanisi," alisema Luhanga.

Akizungumza kuhusu huduma zao za kibenki, Luhanga alisema benki yao imesheheni bidhaa na huduma mbalimbali zenye ubora wa kimataifa ikiwa ni pamoja na akaunti za watoto, mikopo ya nyumba, magari pamoja huduma ya kadi ya mkopo (credit card), ya kipekee nchini inayomwezesha mteja kupata kadi hiyo ikiwa tayari imewekewa kiasi cha pesa cha kuanzia.

Naye Mwenyekiti wa The Runners Club, waandaaji wa Absa Dar City Marathon, Godfrey Mindu, aliishukuru Benki ya Absa pamoja na wadhamini wengine kwani kujitoa kwao kunaenda kuleta mabadiliko makubwa kwa maisha ya Watanzania.

Dar City Marathon 2024 ilishirikisha mbio za Km. 5, 10 na 21 huku kwa upande wa Km. 10 wanawake mshindi wa kwanza alikuwa Anastasia Dolomongo kutoka Arusha akitumia muda wa dakika 34:04:31. Kwa upande wa wanaume mshindi alikuwa Emanuel Shahanga kutoka Hanang akitumia muda wa dakika 29:00:03.

Mbio za Km. 21 (nusu marathon), upande wa wanawake, ushindi wa kwanza ulienda kwa Sara Ramadhani kutoka Arusha pia akitumia muda wa saa 1:13:21:08, huku kwa upande wa wanaume, Dikson Paul kutoka Mwanza akiibuka kidedea kwa kutumia muda wa saa 1:02:58:04.

Mbali na Benki ya Absa kama mdhamini mkuu, wadhamini wengine ni Kampuni ya Alliance Life Assurance, Hill Water, Kilimanjaro Milk na Kampuni ya Garda Security.




Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Absa Tanzania, Aron Luhanga (kushoto), akikabidhi zawadi kwa mshindi wa kwanza wa mbio za nusu marathon (Km. 21) za Absa Dar City Marathon kwa upande wa wanaume, Dickson Paul kutoka Mwanza, baada ya kumalizika kwa mbio hizo jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Absa, Ndabu Lilian Swere. **MPIGAPICHA WETU**

# KMC kukomalia nafasi ya nne

Na Saada Akida

BAADA ya kusuluhu dhidi ya Kagera Sugar, Kocha Mkuu wa KMC FC, Abdihamid Moalin, ameweka wazi kuwa malengo yake na klabu anayoifundisha ni kumaliza katika nafasi tano za juu, kwa sasa akihitaji poiti 15 katika michezo mitano iliyosalia ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

KMC FC juzi ililazimishwa suluhu nyumbani dhidi ya Kagera Sugar, mchezo ukipigwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, kocha huyo alisema kuelekea mwishoni mwa msimu ligi imekuwa na ushindani mkubwa na malengo yao ni kumaliza wakiwa nafasi tano za juu.

Alisema ili kufikia malengo hayo watalazimika kupambana kushinda kila mechi licha ya ugumu wa ligi kwani kila timu kwa sasa inahitaji kufikia malengo huku wengine wakipambania kujinasua katika kushuka daraja.

"Kila mechi kwetu tunahitaji kupata pointi muhimu kwa sababu malengo yetu ni kuona tunamaliza katika nafasi ya nne ambayo tupo kwa sasa, lazima tufanye vizuri katika michezo iliyosalia kuweza kukusanya alama katika kila mechi na si kupoteza zote," alisema Moalin.

Aliongeza kuwa anaimani na vijana wake kufanya vizuri na kufikia malengo hayo ya kuhakikisha wanatafuta pointi katika kila mechi iwe nyumbani ama ugenini.

"Tunaendelea kukisuka kikosi kujiandaa na mchezo wetu ujao, tumekuwa makini katika kila idara safu ya ushambuliaji kutumia nafasi zinazopatikana na ulinzi kutoruhusu bao kwa wapinzani tunanaocheza nao mechi zilizosalia," alisema.

KMC FC inashika nafasi ya nne katika msimamo wa ligi, baadaya kukusanya alama 33, kwa kushinda mechi saba, sare 12, kupoteza sita katika michezo 25 ambayo tayari imeshacheza.

## Simba, Tabora Utd vita vya nafasi leo

INATOKA UK. 24

fikia malengo ya kusaka pointi tatu muhimu.

"Ni kweli tulikuwa na mapungufu kwenye mechi iliyopita na kurudi uwanja wa mazoezi kwa ajili ya kuyapunguza na ikiwezekana kuyaondoa kabisa ili leo tuwe vizuri dhidi ya Tabora United.

„Tunaenda kushindana na washindani wenzetu, mambo mengine tutakuja kujua mwisho wa msimu. Mchezaji yeyote anayesajiliwa na timu basi wajibu wao ni kuitumikia hali ambayo haitakuja kushangaza kuwapo na mabadiliko ya kikosi," alisema Mgunda.

Kocha Msaidizi wa Tabora United, Fabian, alisema maandalizi yamekamilika kwa asilimia 90 na kwamba hawana majeruhi yeyote na waaamini mchezo utakuwa mgumu.

Alisema wanatambua Simba wanahitaji kupata matokeo ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kumaliza nafasi ya pili, lakini pia wao wanataka alama kwa ajili ya kujiondoa nafasi ya chini.

"Presha ni kubwa sana upande wetu kwa sababu ya nafasi tuliyopo, tunataka kupata matokeo mazuri, tumewaangalia Simba ubora wao, tutaingia kwa tahadhari kubwa kuhakikisha tunapata matokeo chanya katika mchezo wa leo," alisema Fabian.

## Yanga bado pointi nane kuwa bingwa

INATOKA UK. 24

ya kulia.

Kipindi cha pili baada ya timu zote kufanya mabadiliko, Mashujaa ilionekana kutawala zaidi, ambapo walifunguka na kucheza mchezo wa kujiachia na kama wachezaji wake wangekuwa makini wangeweza kusawazisha au kupata ushindi.

Alikuwa ni Emmanuel Mtumbuka dakika ya 60, aliyeingia ndani ya eneo la hatari la Yanga na kutazamana ana kwa ana na kipa Djigui Diarra, lakini badala ya kupiga kwa maarifa, alipiga mpira kwa nguvu ukapaa juu la lango.

Dakika mbili baadaye, Zuberi Dabi aliupata mpira uliokuwa umeokolewa ovyo na mabeki wa Yanga, lakini shuti lake lilipita pembeni kidogo ya lango.

Mashujaa ilihamia kwenye lango la Yanga, dakika 15 za mwisho, na nusura isawazishe, pale Juma Nyenyezi alipoupata mpira akiwa nje ya eneo la hatari nakuachia shuti kali la juu lililompita kipa Diarra, lakini badala ya kujaa wavuni uligonga mwamba wa juu na kutoka nje.

Matokeo hayo yanaifanya Mashujaa kuendelea kuwa nafasi mbaya ya 14, ikiwa na pointi 23, ikicheza michezo 25.

Michezo
Jumatatu Mei 6, 2024
Nipashe

**Haaland hazuiliki EPL**
UKURASA 21



# YANGA BADO POINTI NANE KUWA BINGWA

## ●●●Guede azidi kuwaka, sasa wawaachia kazi Simba, Azam mbio nafasi ya pili, lakini...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, sasa wanahitaji pointi nane tu kuweza kutwaa ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo, baada ya jana kupata ushindi mgumu wa bao 1-0 dhidi ya Mashujaa FC, mechi iki-pigwa Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Alikuwa ni straika raia wa Ivory Coast, Joseph Guede, aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili aliyepachika bao pekee katika mechi hiyo ya raundi ya 25.

Guede alisajiliwa kutoka Klabu ya Tuzlaspor ya Uturuki, alifunga bao hilo akimalizia kazi nzuri iliyofanywa na Mudathir Yahya na kutimiza bao la sita kwenye orodha ya wafungaji.

Lilianzia kwa Stephane Aziz Ki, aliyeupata mpira kwenye wingi ya kulia, akawahadaa mabeki wa Mashujaa waliokuwa wanamfuata, akausogeza mpira mbele kwa Mudathir aliyekuwa karibu na mstari wa mwisho wa uwanja, alichofanya ni kugeuka na kumtazama Guede ambaye alikuwa hajakabwa na mtu yeyote, akapiga krosi ya kuurudisha mpira ndani, mfungaji kazi ikawa rahisi tu ya kuudokoa, mpira ukajaa wavuni.

Ushindi huo unaifanya Yanga kufikisha pointi 65, ikibakisha mechi tano tu kabla ya kumaliza msimu, lakini ikihitaji pointi nane ili kufikisha pointi 73 ambazo hazitoweza kufikiwa na timu yoyote.

Katika mechi tano ilizobakiza nazo, inahitaji kushinda mechi tatu, au kupata ushindi mechi mbili na sare mbili.

Takwimu zinaonyesha kuwa iwapo Azam FC iliyo nafasi ya pili itashinda mechi zake sita ilizosaliwa nazo itafikisha pointi 72, huku Simba iliyo nafasi ya tatu kama ikishinda michezo yake saba iliyobaki nayo, itafikisha pointi 71 tu.

Mchezo wa jana ulianza kwa Mashujaa ‚kupaki basi‘, huku wakiwaruhusu wachezaji wa Yanga kuwa na mpira muda mwingi wa mchezo na wao kutaka kushambulia kwa kushtukiza, kitu ambacho hata hivyo hakikuwezekana katika kipindi cha kwanza.

Ilipofikia dakika ya 25, Mashujaa walionekana kubadilisha mfumo na kuanza kuondoka langoni mwao, wakiamua kuwabana Yanga kwenye eneo lao, na papo hapo wote walirudi nyuma walipokuwa wakishambuliwa.

Mifumo yote miwili haikufanikiwa kwani, ilifanya shambulizi moja tu kwa dakika zote 45, wakati Adam Adam alipoingia ndani ya eneo la hatari dakika ya 29, akitokea wingi ya kushoto, lakini alijikanyanga mwenyewe badala ya kufanya maamuzi, mabeki wa Yanga wakauchukua mpira kiulaini.

Mudathir kama angekuwa makini, angeweza kuipatia Yanga mabao mawili, dakika ya 24, na 28, lakini mara zote alikosa utulivu na maamuzi sahihi ya kuweka mpira ndani ya nyavu.

Faulo iliyopigwa na Aziz Ki, dakika ya 30 nusura iende moja kwa moja wavuni kama Omari Kindamba asingepiga kichwa mpira ambao ulitoka juu ya lango na kuwa kona.

Faulo hiyo ilitokana na Yao Kouassi kuangushwa pembeni mwa uwanja, ndani kidogo ya kibendera cha wingi

INAENDELEA UK. 23



Stephane Aziz Ki, akimpongeza Joseph Guede kwa kumbeba na kushangilia pamoja baada ya kuifungia Yanga bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya Mashujaa FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma jana. **PICHA: YANGA**

# Simba, Tabora United vita vya nafasi leo

**Na Saada Akida**

POINTI tatu, ndiyo wimbo unaoimbwa na makocha Juma Mgunda wa Simba na Ben Fabian wa Tabora United, kuelekea mchezo wa leo ambapo kila mmoja akiwa na malengo yake.

Wekundu wa Msimbazi wanazihitaji alama hizo kwa ajili ya kusaka nafasi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara wakati Tabora United wakizitaka pointi hizo ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kujinasua kutoka nafasi ya chini ya kwenye msimamo na kusalia Ligi Kuu msimu ujao.

Timu hizo mbili leo zinakutana kwa mara ya pili msimu huu, Simba wakiwa wenyeji wa mchezo huo wakiwakaribisha Tabora United, Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi jijini Dar es Salaam, saa 12:15 jioni.

Simba wataingia dimbani wakiwa nafasi ya tatu kwenye msimamo na alama 50 baada ya kucheza michezo 23 wakiwa na mchezo mmoja mkononi na Tabora United ambayo ipo nafasi ya 15 wakikusanya pointi 23 kwa michezo 24 ambayo tayari imecheza.

Wekundu wa Msimbazi hao wanaingia uwanjani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi katika mchezo uliopita wa ligi hiyo baada ya kuichapa Mtibwa Sugar mabao 2-0, wakati Tabora United wakitoka kupokea kichapo cha mabao 3-0 mbele ya Yanga katika mchezo wa robo fainali ya Kombe la Shirikisho la CRBD Bank.

Kwa msimu huu timu hizo zimekutana mara moja katika ligi tu na Simba kufanikiwa kushinda mabao 4-0 dhidi ya Tabora United wakiwa nyumbani katika dimba la Al Hassan Mwinyi, Tabora.

Kuelekea mchezo huo, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Mgunda alisema maandalizi yameenda vizuri dhidi ya Tabora United na haijalishi wanakutana na timu ipo kwenye nafasi gani.

Alisema hakuna mchezo rahisi katika Ligi Kuu na hawaangalii wako katika hali gani zaidi ya kuandaa timu yao kwa ajili ya kushindana nao na ku-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >